# Nipashe

Jumatano Novemba 25, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580410

www.ippmedia.com

MWANGA WA

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 10

FOLLOW US




**MAGUFULI** awateua Dk. Shein, Kabaka na Dk. Mwakyembe



UKURASA 7

**TANZANIA** yateuliwa uenyekiti kamati UN

UKURASA 5

**Pirlo: Ronaldo hapewi kipaumbele hapa Juventus**

UKURASA 20

# HATIMAYE

• **Wabunge** Viti Maalum CHADEMA wala kiapo, Mdee atoa neno, Ndugai aanika kila kitu... *Endelea ukurasa 2*



SALOME MAKAMBA

ESTER BULAYA

SOPHIA MWAKAGENDA

ESTHER MATIKO

Aliyekuwa Mbunge wa Kawe kupitia CHADEMA, Halima Mdee, akiapa mbele ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, jijini Dodoma jana, kuwa mbunge wa viti maalum kwa tiketi ya chama hicho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WAFUNGUKA BARUA YA RAIS ACT- WAZALENDO**

ZIKIWA zimepita siku saba tangu Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kukiandikia barua Chama cha ACT-Wazalendo, wachambuzi wa siasa...

UKURASA WA 5

**SIRRO ATAJA KIINI SHULE KUTEKETEA KWA MOTO**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, imebainika kuwa mfululizo wa matukio ya shule kuteketea kwa moto yanasababishwa na mambo mengi...

UKURASA WA 7

**WAHUKUMIWA FAINI KWA KUTUMIA MTANDAO KILAGHAI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu Baraka Mtunga na Rajabu Katunda kulipa faini ya Sh. milioni tatu au...


RIPOTI MAALUMU

## Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo watoto -3

UKURASA 4

## TAMISEMI yachunguza udanganyifu mitihani

UKURASA 2


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



**MICHEZO** **MUUAJI SIMBA AENDELEA KUTAKATA** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mafundi wakichanganya zege kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Shule ya Sekondari Kiriba iliyopo Wilaya ya Musoma mkoani Mara, juzi. Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule hiyo, Paul Mtani (hayupo pichani), serikali imetoa Sh. milioni 50 kuchangia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatimaye waapishwa

**Na Waandishi Wetu**

WABUNGE 19 wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamekula kiapo cha ubunge jana huku wakisema wana baraka zote kutoka kwenye chama chao na watafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu na kwa kiwango kilekile cha Bunge la 11.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika akizungumza na Nipashe jana, alisema chama hicho kitachukua hatua baada ya wabunge hao kuapishwa.

"Nasisitiza tu kwamba, Katibu Mkuu sikuwasilisha orodha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wala Bunge, pili Kamati Kuu ya chama, haikuteua wabunge wa viti maalumu, tatu, tutakaa kwenye vikao vya chama tutaeleza hatua ambazo tutazichukua," alisema Mnyika.

Awali, katika ukurasa wake wa twitter, kabla ya wabunge hao kuapishwa, Mnyika aliandika kuwa; kwa upande wa chama aliandika barua NEC kuwajulisha kuhusu viti maalum kwa chama hicho.

"Status kwa upande wa CHADEMA, na kwa katibu mkuu ni hii hii ya Novemba 8, mwaka huu na niliandika barua kwa kuwajulisha. Tunafuatilia yanayojiri ofisi ya Spika wa Bunge na kuthibitisha hujuma au usaliti, hatutasita kuchukua hatua. Turejee kwenye mjadala," aliandika Mnyika kwenye ukurasa wake jana.

### KAULI YA MDEE

Akizungumza kwa niaba ya wabunge hao baada ya kuapishwa katika Viwanja vya Bunge na Spika wa Bunge Job Ndugai, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA), Halima Mdee, alikishukuru chama hicho chini ya Mwenyekiti Mbowe kwa kuwapa nafasi hiyo.

"Tunashukuru kupitia wao wametupa nafasi hii ya kuwakilisha chama chetu ambacho kwa mujibu wa matakwa ya sheria za nchi, kimekidhi kigezo cha kupata viti maalum, kwa hiyo viti hivi sio hisani ila ni sehemu ndogo ya ushindi mkubwa ambao chama chetu kimepata," alisema.

Mdee alimhakikishia Spika Ndugai kwamba kama anavyomjua vizuri, wamefanya kazi wote kwa miaka 10 na watafanya kazi kwa uaminifu kama kambi ya upinzani bungeni.

"Tutafanya kwa uadilifu mkubwa na kwa viwango vile vile ambavyo tumekuwa tukivifanya, tuwahakikishie watumishi wa bunge hapa kuna vijana wapya kwenye chama tuwahakikishie sisi kama dada zao tutahakikisha wanafanya kazi bora na nzuri kwa ajili ya taifa na nchi kwa ujumla," alisema.

### KAULI YA MATIKO

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, alipoulizwa kuhusu kupewa idhini na chama kula kiapo alisema "Kama mnavyofahamu utaratibu za ubunge viti maalum hadi kufika kuteuliwa, taratibu zinaendelea ndani ya chama na baadaye chama kikabariki kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi, binafsi nilitaarifiwa kuteuliwa ndio maana nikaja hapa kula kiapo. Nilitaarifiwa na mamlaka husika."

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu kauli ya Mnyika, alisema: "Sijui zaidi ya hapo kifupi najua nimetaarifiwa na naendelea kukishukuru chama kimeona kimepata nafasi chache sana 19, lakini kimeona katika hao 19 basi na mimi niwepo kukitumikia chama na taifa."

Alisema kwa uchache wao wanawahakikishia Watanzania wategemee makubwa kutoka kwao.

"Tunajua yaliyojiri kwenye uchaguzi, tumepata hiki kidogo kwa ushindi mkubwa tulioupata, kwa hiyo ni fursa ya pekee ambayo tutatumia kwa nguvu zote, akili zote tunakiwakilisha chama vizuri ndani na nje ya bunge, lakini tunawatetea Watanzania ambao wengi wao wana imani na sisi," alisema.

Kadhalika alipoulizwa msimamo wao endapo chama kitawafuta uanachama, Matiko alisema "Tupo hapa kwa sababu ya chama, hivyo chama kikiona kuna mwingine anafaa zaidi, Matiko nipo tayari. Sasa kama kuna mengine yalienda yakarudi yatazungumzwa kwa wakati muafaka leo (jana) ni kula kiapo."

### NDUGAI

Akizungumza baada ya kuwaapisha, Spika Ndugai alisema Novemba 20, mwaka huu alipokea barua kutoka NEC ikieleza kuteua wabunge 19 wa viti maalum wa chama hicho.

Hata hivyo, alifafanua kuwa kwa mujibu wa ibara ya 78(1) ikisomwa na ibara ya 66(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaeleza vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi mkuu kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kupata angalau asilimia tano ya kura zote halali za wabunge, vitapendekeza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia uwiano wa kura.

Pia alisema ibara ya 78(3) ya Katiba inaweka masharti kwamba majina ya watu walipendekezwa kwa mujibu wa ibara ya 78(1) na NEC yatatangazwa kama matokeo ya uchaguzi baada ya NEC kuridhika kwamba masharti ya Katiba na sheria yanayohusika yamezingatiwa.

Alisema vyama mbalimbali vilivyoshiriki kwenye uchaguzi mkuu 2020 kimojawapo ni CHADEMA na kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi yaliyotolewa na NEC chama hicho kimefikia idadi ya kura zinazowezesha kupata wabunge wa viti maalum.

Akifafanua sababu ya kuapishwa nje ya mkutano wa Bunge, Ndugai alisema kanuni ya 30(b) ya Kanuni za Bunge inatoa ufafanuzi zaidi kuhusu kiapo cha wabunge kwa kipindi ambacho kunakuwa hakuna Mkutano wa Bunge unaoendelea.

"Kama hakuna mkutano wa bunge unaoendelea kanuni inaeleza kuwa 'Bila kujali masharti ya fasili ya kwanza endapo mbunge atachaguliwa au kuteuliwa baada ya uchaguzi mkuu Spika atamwapisha katika eneo litakalopangwa na Spika iwapo hakuna mkutano na baadaye atatoa taarifa bungeni kwenye kikao cha kwanza cha mkutano wa bunge unaofuata," alisema.

Ndugai alisema utaratibu huo mpya umetokana na Bunge la 11 lililopita kuona ipo haja ya kutatua tatizo la wabunge wanaochaguliwa au kuteuliwa kuchelewa kuanza kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya kusubiri kuapishwa.

Alisema lengo la utaratibu huo ni kuhakikisha wanaapishwa pasipo kuchelewa na kuwawezesha kuanza kutekeleza majukumu ya Bunge katika kufanikisha matarajio ya wananchi waliowaamini na kuwaletea maendeleo.

Alisema walioapishwa ni wabunge kamili na wana haki zote kama wengine hivyo kuwatakia kila la heri kwenye safari mpya ya miaka mitano.

### SURA MPYA TANO

Kati ya wabunge 19 walioapishwa, wabunge watano ni wapya.

Wabunge wapya ni Agnesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau na Stela Fiyao.

Wabunge wengine 14 ambao walikuwepo bunge lililopita ni Halima Mdee, Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Paresso, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

***IMEANDALIWA na Augusta Njoji (DODOMA) na Christina Mwakangale(Dar es Salaam).***

## TAMISEMI yaanza uchunguzi wa udanganyifu wa mitihani la saba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza uchunguzi wa udanganyifu uliofanyika kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka huu huku ikiahidi kuchukua hatua kali kwa wale wote waliohusika.

Udanganyifu huo umesababisha wanafunzi 1,059 katika shule 38 kufutiwa matokeo kutokana na tuhuma hizo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Jijini hapa, Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamhanga, alisema uchunguzi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya wiki moja na hatua kali zitachukuliwa kwa wahusika wote.

"TAMISEMI inalaani vikali tabia hii ya kukiuka taratibu za ufanyikaji na uendeshaji wa mitihani ya kitaifa, na uchunguzi unaendelea na endapo kuna watumishi wa serikali au sekta binafsi watabainika kuhusika serikali itachukua hatua kali,"alisema.

Alisema serikali itachukua hatua ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia hiyo.

"Wote lazima wabebe mzigo huo hatupendi hivi vitu vitokee na hatukubali. Tumeanza uchunguzi na unafanyika kupitia Ofisi za Mikoa na Wilaya, kwa upande wa shule za binafsi zilizohusika kunafanyika utaratibu wa kujiwajibisha utakuwa tofauti," alisema.

Kuhusu mtihani wa kidato cha nne inayoendelea hadi Desemba 11, mwaka huu, Mhandisi Nyamhanga alizitaka kamati za mitihani za mikoa na halmashauri, kuhakikisha unafanyika kwa amani, utulivu na usalama ili kupata matokeo yaliyokusudiwa.

Aliagiza uendeshaji na usimamizi wa mitihani ufanyike kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za Baraza la taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) na endapo itabainika kuna ukiukwaji wa sheria, hatua kali za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa wahusika.

Pamoja na hayo, aliwaagiza viongozi wa mikoa na halmashauri kukamilisha maandalizi yote yanayotakiwa kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wa shule za awali na darasa la kwanza watakaoanza masomo Januari, mwakani.

"Pia hawa viongozi wakamilishe miundombinu, samani na kuweka mazingira mazuri kuwapokea wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza bila vikwazo vya aina yeyote ili kutekeleza sera ya utoaji wa rlimu msingi bila malipo,"alisema.

Nyamhanga alisema kwa sasa shule inafanya maandalizi ya kujenga shule za sekondari maalum za wasichana zenye hadhi ya kitaifa kila Mkoa ikiwa ni kuboresha mazingira ya watoto wa kike kupata elimu.

## HABARI KITAIFA

# Wafunguka barua ya Rais kwa ACT- Wazalendo

**Na Romana Mallya**

ZIKIWA zimepita siku saba tangu Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kukiandikia barua Chama cha ACT-Wazalendo, kuomba jina la Makamu wa Kwanza wa Rais, wachambuzi wa siasa wamesema Rais haondolewi mamlaka ya kufanya kazi zake hata wasipotekeleza agizo hilo.

Novemba 19, Rais Mwinyi wakati akitangaza Baraza la Mawaziri aliloliunda, alisema ameiandikia ACT-Wazalendo kuomba jina la mtu wa kujaza nafasi hiyo ikiwa ni takwa la kikatiba.

Katiba inasema chama kinachofikisha zaidi ya asilimia 10 ya kura, kinajumuishwa katika kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) na kinapewa siku 90 kupeleka jina ikiwa hakifanya hivyo katika siku saba za mwanzo.

Wakizungumza na Nipashe jana, wachambuzi wa kisiasa walisema suala kama hilo la upinzani kutopeleka jina hakumwondolei Rais kutekeleza majukumu yake.

Juzi, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, wakati akihojiwa na chombo kimoja cha nje kuhusu barua hiyo, alisema hawakuijibu kutokana na msimamo wao wa kutokubaliana na matokeo ya uchaguzi.

Mchambuzi wa kisiasa, Othman Masoud, alisema katiba iko wazi kuwa kama ACT-Wazalendo itashindwa kupeleka jina hilo ndani ya siku 90, Rais anaweza kuacha kumteua Makamu wa Kwanza wa Rais na kuteua nafasi mbili za mawaziri zilizobaki.

"Kisheria hakuna madhara yoyote ya kiutendaji ila itategemea namna mtu atakavyoitafsiri kwa sababu kifungu cha 91 (2) (f) cha katiba hiyo kinasema Rais anaweza kuteua mawaziri wawili lakini nafasi ya makamu ikawa haina mtu.

"Ukiangalia kwa muundo wa kiserikali unakuwa haujakamilika na unaweza kusema hauko halali na mwingine akasema uko halali kwa sababu una Makamu wa Pili wa Rais, lakini hauna Makamu wa Kwanza.

"Kuna kifungu cha katiba kinaeleza uwiano uliopo ndani ya Baraza la Wawakilishi, hauiwezeshi serikali kuwa halali, kwa hivyo Rais anatakiwa avunje baraza na kuitisha uchaguzi upya," alisema.

Mchambuzi huyo alisema kama ilivyotokea uchaguzi wa mwaka 2015 baada ya matokeo kufutwa na uchaguzi kurudiwa upya na baadaye CCM kutangazwa kimeshinda na upinzani kususia, Rais aliendelea kutekeleza majukumu yake.

"Lilikuwapo katika awamu iliyopita na bahati mbaya mtu hawezi kwenda mahakamani kupinga kwa sababu imekatazwa na kifungu cha 10 (a) cha katiba yenyewe.

"Lakini, kisiasa unaweza kusema madhara yake ni hayo, tukiangalia katiba ya Zanzibar imeundwa kwa misingi ya kifungu cha 9 chini ya maridhiano, ukiwa hauna unajiuliza, je, umetimiza matakwa ya katiba?

Mchambuzi huyo alisema Makamu wa Kwanza wa Rais katika serikali ya umoja wa kitaifa, hana mamlaka lakini ana kazi za kufanya.

"Kwa sababu anawakilisha upande wa pili wa chama cha upinzani, unajua mazingira ya Zanzibar tulikotokea kulikuwa na mgawanyiko tulikuwa tunaona ni 100, labda 50 kwa 50 na sasa umepungua na umekuwa mkali zaidi," alisema.

Pia alisema Makamu wa Kwanza wa Rais hana mamlaka ya kuteua, kufukuza wala kufanya uamuzi wowote zaidi ni kushauriana na Rais kama inavyofanyika upande wa Tanzania Bara.

Naye, Prof. Abdallah Safari alisema endapo siku 90 zikiisha na ACT-Wazalendo wasipopeleka jina, maana yake kutakuwa hakuna serikali ya mseto.

Alisema kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais, hana mamlaka yoyote ni kama alama tu imewekwa.

Katika mahojiano hayo ya juzi, Zitto alisema suala hilo linajadiliwa katika ziara ya Mwenyekiti wa Chama Maalim Seif ambaye anatembelea waathirika wa matukio ya uchaguzi.

Alisema hawatapeleka jina kwa sababu hawakukubali uchaguzi na kama chama wana michakato ya demokrasia na uamuzi ulishapitishwa kuwa hawautambui.

Awali, Maalim Seif, alikiri kupokea barua hiyo kuhusu kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kueleza kuwa chama hicho kipo kwenye mashauriano.

**MARIDHIANO**

Mwaka 2010 kulifanyika maridhiano visiwani humo baina ya Rais Amani Abeid Karume na Maalum Seif wakati huo akiwa Chama cha Wananchi (CUF). Katika maridhiano hayo, Makamu wa Kwanza wa Rais moja ya kazi zake ni kuwa Mshauri Mkuu wa Rais.

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, Rais Mwinyi alipata jumla ya kura 380,403 sawa na asilimia 76.27 na Maalim Seif Shariff Hamad, mgombea kupitia ACT-Wazalendo, alipata kura 99,103 sawa na asilimia 19.87.

Baada ya matokeo hayo kutangazwa ACT-Wazalendo kiliyagomea na kudai uchaguzi haukuwa huru na haki.

**UCHAGUZI 2015**

Siku moja baada ya uchaguzi mkuu kufanyika mwaka 2015, Maalim Seif alijitangaza mshindi na ndipo Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jecha Salim Jecha, alifuta matokeo ya uchaguzi huo akisema haukuwa wa haki na ulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu za uchaguzi.

Uchaguzi huo ulirudiwa, lakini baada ya matokeo kutangazwa, CUF kilisusia matokeo hayo hivyo CCM kiliongoza serikali bila ya kuwa na Makamu wa Kwanza wa Rais.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)
BODI YA MAJI YA WADHAMINI LYAMUNGO - UMBWE (LUWST)
S. L. P. 8365, Moshi. Simu: +255 710 666500 baruapepe: lyamungoumbwe@yahoo.com

## VACANCY FOR WATER TRUST MANAGER

Lyamungo – Umbwe Water Supply Trust (LUWST) under RUWASA is a full autonomous Water Utility isresponsible for the provision of adequate clean and safe drinking water and improvement of hygienic situation. LUWST is looking for a dynamic, results driven individual to fill in the position of **"Manager"**

1. **Purpose of the Job**
   This is a Managerial position in which the position holder will be responsible with the entire managerial aspects of water supply, **community hygienic proportion and sound environmental affairs** as well as Human Resources management.

2. **Main duties and Responsibilities**
   i. The Chief Executive of Trust responsible for administrative issues on day to day basis,
   ii. Responsible to prepare annual budgets and recommend staffing levels required for the Trust and submits them to the Board for approval,
   iii. Regularly review actual performance against approved plans and budgets and submit reports to the Board detailing recommendations for actions necessary to correct adverse variance,
   iv. Responsible to ensure all Trust's financial transactions are authorized and controlled in accordance with the agreed procedures and that proper system of internal control is maintained,
   v. Responsible for preparing and submits to the external Auditor the annual accounts of the Trust within four months after the end of the financial year,
   vi. Responsible for maintaining and repairing, planning and construction of both extension and new water projects.
   vii. Recommend new or amendment of polices, regulations and by-laws to the Board for:
   - Fixing water tariffs and revenue collections,
   - Control and properly manage all assent of Trust as per public property management guides
   viii. To perform any other duties as may be assigned by the Board and Government Official as per Trust's constitution and Memorandum of Understand

3. **Minimum Job Requirements**
   **3.1. Qualification**
   - First degree in Engineering in any of the following disciplines; Civil, Mechanical, Environmental or any Water Related Discipline (Master Degree in water resources Management will be an added advantage).
   - Should be registered as ProfessionalEngineering with Professional Engineer Board and have more than Five years of relevant working experience, of which three years must be in senior management position,
   - Should have a background in water supply utility or related engineering aspects as well as have analytical, broad minded, creative and unquestionable integrity,
   - In service employer with Diploma in water supply and sanitation or equivalent qualification with extensive proven working experience may apply.

   **3.2. Key competence**
   - Proven computer knowledge and skills,
   - Demonstrated good leadership qualities,
   - Ability to work in team work and under pressure
   - High level of initiative, creativity and integrity

4. **Age Limit**
   The applicant should be below 50 years when lodging this application

5. **Nature of Employment**
   Five years (5) renewable contract depending on the performance

6. **Remuneration**
   This position attracts competitive salary plus other fringe benefits

7. **Mode of Application**
   A hand written application along with Curriculum Vitae to include reliable contacts (emails and day time working telephone), applicant's recent passport size photo and copies of all relevant certificates, transcripts and testimonies, names and addresses of at least three (3) reputable referees to **reach the undersigned by 21st December, 2020 before 15:30 hours**

**Chairman,**
**Lyamungo – Umbwe Water Supply Trust (LUWST)**
**P.O.Box 8365,**
**Moshi – Kilimanjaro**

# Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo vya watoto -3

**Na Elizabeth Zaya**

***SEHEMU ya tatu na ya mwisho ya ripoti hii maalum inaeleza jinsi ugonjwa wa corona ulivyoathiri vituo vya watoto yatima kutokana na wafadhili kusitisha misaada, wasimamizi wa vituo hivyo wanavyohangaika ili watoto wao wasikose haki ya elimu, chakula, mavazi na sehemu ya kulala na kauli iliyotolewa na serikali.***

Mmiliki wa kituo cha kulelea watoto cha Ikwiriri, Kazamoyo mkoani Pwani, anasema jengo ambalo watoto hao wanaishi ni la kupanga na mpaka sasa wana muda wa miezi saba hawajalipa kodi.

"Tumezungumza na mmiliki wa nyumba ametupa muda tujipange tumlipe, kwa hiyo hilo nalo ni tatizo jingine linalotusumbua ukiacha kuwaza namna gani tunapata pesa kwa ajili ya chakula na huduma nyingine za watoto," anasema.

Mwenyekiti wa vituo vya kulelea watoto yatima Wilaya ya Kinondoni, Hassan Hamisi, anasema alikuwa anapokea malalamiko mengi kutoka kwa wamiliki wa vituo vilivyopo katika wilaya yake baada ya hali kuzidi kuwa ngumu na kutokuwa na uhakika wa malezi bora kwa watoto katika vituo vyao.

"Ni kweli hali ilikuwa ngumu sana na bado haijatengamaa vizuri kwa sababu kila mmoja alikuwa anakuja analalamika kwa lengo la kuomba angalau msaada wa ushauri namna ya kufanya katika kipindi hicho kigumu," anasema Hamisi.

Hamisi anasema eneo kubwa ambalo vituo vingi viliathirika zaidi ni upande wa chakula kwa watoto. Anasema baada ya hali kuzidi kuwa mbaya na wahisani ambao walikuwa wanasaidia vituo vingi kutoka nje ya Tanzania kusitisha misaada yao, walilazimika kuandika barua na kusambaza katika taasisi mbalimbali nchini kuomba msaada.

"Lakini ninavyozungumza na wewe hivi karibu zote hazikutujibu, isipokuwa juzi tu kuna benki moja hivi ndiyo ilitujibu," anasema Hassani.

### AFYA TETE

Hamisi anasema anamiliki pia kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (CHAKUWAMA), kilichopo Kijitonyama.

Anasema kituo hicho pamoja na kuathirika katika maeneo mengi, lakini upande wa afya ndiyo kiliathirika zaidi.

"Hali ilikuwa mbaya katika maeneo mengi kwa sababu misaada yote ilisitishwa tukabaki tunatumia akiba tuliyokuwa nayo tu, lakini hali ilikuwa mbaya zaidi katika kuwahudumia watoto kiafya, kwa sababu hilo nalo tulikuwa tunasaidiwa na wahisani."

"Wapo baadhi ya watoto ambao walikuwa na bima ya afya kwa hiyo walitumia hiyo, lakini kuna baadhi ambao hawakuwa nayo kwa hiyo tulifika mahali tunakosa hata pesa ya kununua dawa."

Hamisi anasema mpaka sasa hali bado haijarudi katika hali yake ya kawaida japokuwa ni mtu mmoja mmoja wa ndani ya nchi ndiyo wanaowatembelea.

"Kwa sababu kama unavyojua baadhi ya nchi bado zinaendelea kukabiliwa na huu ugonjwa wa corona, kwa hiyo bado hawajaanza kutoka sana nje ya nchi zao," anasema Hamisi.

"Serikali yetu imeendelea kuwahakikishia kwamba nchi yetu iko salama na namna ambavyo imepigana na hii vita, tunaamini wataanza kuja na hali itarejea katika hali ya kawaida."

### KAULI YA SERIKALI

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prudance Costantine, anasema hawajapata malalamiko yoyote kutoka kwa wamiliki wa vituo hivyo kuyumba.

Ugonjwa huo wa corona uliripotiwa kwa mara ya kwanza Desemba 31, mwaka jana nchini China, katika mji wa Wuhan na Tanzania uliripotiwa Machi 16, mwaka huu.

Nchi nyingi zilifunga mipaka yao na kuzuia watu kusafiri na nyingine raia wake walilazimishwa kujifungia (lockdown) ili kudhibiti usiendelee kusambaa na kuleta athari zaidi.

### ATHARI YA CORONA

Ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa Novemba 10, mwaka huu kutoka Roma nchini Italia na Geneva, Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa yakihusisha la Uhamiaji (IOM) na Mpango wa Chakula Duniani (WFP), inaeleza kwamba madhara ya kiuchumi na kijamii yanayosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona yanatisha kuliko janga lenyewe.

Ripoti hiyo inafafanua kwamba vikwazo vya kutembea ili kuepusha kusambaa zaidi kwa ugonjwa huo katika nchi zaidi ya 200 vimeathiri kwa kiwango kikubwa uchumi na jamii na kuonya kuwa huenda yakawa makubwa zaidi na hivyo kutoa wito kwa dunia kuchukua hatua za haraka ili kukidhi mahitaji ya kibinadamu yanayoongezeka na kushughulikia athari hizo bila kusahau walio katika hatari zaidi.

Pia inaonyesha kuwa, janga hilo limeongeza ukosefu wa chakula na kuweka hatarini zaidi wahamiaji, walio kwenye mizozo na majanga pamoja na familia zinazotegemea upokeaji wa fedha kutoka kwa jamaa (wahisani).

Mkuu wa Kituo cha Kulelea Watoto Yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (Dogodogo Center), Kilichopo Bunju A, jijini Dar es Salaam, Dk. Dyfrig Maliti, anasema mipango yote ambayo wahisani kutoka nje walikuwa wameahidi kuwasaidia imevurugika.

Anasema kabla ya kuzuka kwa ugonjwa huo, kulikuwa na mipango mingi ya kuendeleza kituo hicho ambayo wahisahi katika nchi mbalimbali waliahidi, lakini mpaka sasa imekwama.

Dk. Maliti, anasema miongoni mwa miradi iliyositishwa ni pamoja na ujenzi wa shule ya sekondari.

### WAPONEA KANISANI

Dk. Maliti anasema kwa upande wa chakula, amekuwa akitumia mbinu ya kuomba msaada katika siku za ibada kwa waumini kuwasaidia kuchangia chochote walichonacho.

"Kati ya vipindi ambavyo sitamani kukumbuka ni hiki cha corona tulichopitia, mimi ni mtumishi wa Mungu, kwa hiyo huwa ninapokwenda kanisani, natumia muda wa baada ya ibada kuwaambia watu ukweli kuhusiana na hali tunayopitia,"

"Hatuna chakula, na hawa watoto ni wetu sote, tunawasaidiaje...kwa hiyo kama kuna mtu mwenye chochote anatusaidia, tunavuka kwa mtindo huo, japokuwa sisi hapa kwetu huwa tunashughuli mbalimbali tunafanya ikiwamo kulima mboga zetu wenyewe kwa ajili ya chakula, hilo nalo linasaidia. Ila hali bado si shwari sana."

Kwa upande wa afya kwa watoto wanaoishi katika kituo hicho, Dk. Maliti anasema mpaka sasa wanaomba Mungu ili wasiugue kwa sababu hilo ni eneo ambalo walikuwa wanasaidiwa na wahisani wa nje ya Tanzania.

"Tunaomba Mungu atusaidie watoto wasiugue kama ambavyo mpaka sasa ametusaidia, maana hawana bima ya afya, matibabu walikuwa wanatusaidia wenzetu wa nje ambao hatujui lini na wao watakuwa huru na huu ugonjwa wa corona kama ilivyo sisi Tanzania," anasema Dk. Maliti.

HABARI KITAIFA

# Sirro ataja kiini shule kuteketea kwa moto

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amesema mfululizo wa matukio ya shule kuteketea kwa moto wamebaini inasababishwa na mambo mengi ikiwamo migogoro ya uongozi kwenye taasisi hizo.

Alisema hayo juzi wakati akihojiwa kuhusu hali ya usalama nchini kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV kila ya Jumatatu.

IGP Sirro (pichani chini) alisema katika uchunguzi uliofanywa na jeshi hilo, wamebaini kuwa kila tukio lina sababu zake, hivyo hakuna sababu ya jumla.

Alisema matukio mengi yanatokana na migogoro ya uongozi kwenye taasisi kutokana na maslahi binafsi katika baadhi ya shule.

Alisema sababu ya pili ni baadhi ya shule kuwa na miundombinu ya umeme na majengo ambayo haijawekwa vizuri.

IGP Sirro alisema tatizo la tatu ni hujuma ambapo mwalimu anaona haelewani na utawala, hivyo anamua kumtumia mwanafunzi akachome shule.

Kimsingi, kila tukio linatokana na sababu zake, na wala hakuna sababu za jumla wala hakuna sababu inayotokana na mambo ya siasa au mambo ya dini...wengine wanasema mwalimu alikuwa ananifundisha ananipiga tu viboko, anaamua kwenda kuchoma magodoro," alisema.

IGP Sirro alisema kutokana na sababu hizo, Jeshi la Polisi limetoa maelekezo awe anaachwa mwanafunzi mmoja bwenini, kila shule kuwe na ulinzi na kujenga uzio ili kupunguza matukio hayo.

Septemba mwaka huu, wanafunzi 10 walifariki dunia kwa ajali ya moto ulioungunza bweni la wavulana katika Shule ya Msingi Byamungu iliyopo wilayani Kyerwa mkoani Kagera.

Julai pia kulishuhudiwa matukio makubwa mawili ya moto yakizigusa shule mbili tofauti ambazo zinamilikiwa na dhehebu la Kiislamu.

Tukio la kwanza lilikuwa ni wanafunzi watatu wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari ya Islamic iliyopo Ilala Dar es Salaam walipoteza maisha baada ya shule hiyo ya bweni kuungua moto.

Pia shule ya The National Muslim Council of Tanzania inayomilikiwa na Kinondoni High School pamoja na Kinondoni College School iliyopo jijini Dar es Salaam iliungua moto yote na kusababisha hasara kubwa.



Wiki iliyopita, shule ya wasichana ya Loreto mkoani Mwanza nayo iliteketea kwa moto na kusababisha hasara kubwa kwa wanafunzi.

# Tanzania yateuliwa uenyekiti kamati UN

**Na Waandishi Wetu**

TANZANIA imeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hati za Utambulisho ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN Credentials Committee) New York Marekani kwa mwaka 2020/2021.

Hii ni mara ya kwanza katika historia ya Tanzania kushika nafasi ya kuongoza kamati hiyo nyeti ya UN, na kwamba uteuzi wake ulipendekezwa na Ofisi ya Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kuidhinishwa kwa kauli moja na wajumbe wote tisa wa kamati hiyo.




Wajumbe hao ni Marekani, China, Urusi, Cameroun, Uruguay, Iceland Papua Guinea, Trinidad na Tobago-na na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza mara baada ya uteuzi huo Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika UN, Balozi Prof. Kenedy Gaston, alisema uteuzi huo ni muhimu na ni ishara ya namna nchi inakubalika katika uso wa Jumuiya ya kimataifa.

Alisema kukubalika kwa Tanzania ni kutokana na uongozi thabiti wa halikadhalika sera zake za mambo ya nje.

Balozi Prof. Gaston aliongeza kuwa kwa mara ya kwanza tangu uteuzi huo Tanzania imeongoza kikao chake cha kwanza cha kamati hiyo kilichofanyika New York, Marekani.


TRA

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

## TAARIFA KWA UMMA

### WITO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA USAFIRISHAJI WA ABIRIA KWA MASAFA MAREFU

***Dar es Salaam, Novemba 24, 2020:***

Itakumbukwa kuwa tarehe **29 Mei 2020**, Serikali, kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na baadhi ya Wamiliki wa Mabasi ya Abiria wa Masafa Marefu, ilizindua Mfumo wa Tiketi Mtandao. Lengo ni kuboresha huduma ya usafiri kwa abiria wa masafa mrefu, kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, kuwahakikishia wamiliki wa vyombo vya usafiri kupata mapato yao stahiki na kwa wakati. Mfumo huo, ambao umejengwa na wataalam wetu wa ndani na kwa mujibu wa Sheria, kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kanuni ya 22(j) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020,** zilizotengenezwa kutokana na matakwa ya **Kifungu cha 45 cha Sheria ya Usafirishaji, SURA 317**, umeiwezesha TRA kuwa na Mfumo wake, ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya **Kifungu cha 35 cha Sheria Usimamizi wa Kodi, SURA 438**, ili kuongeza ufanisi na uwazi wa kupata taarifa sahihi za kisekta kwa ajili ya kuisaidia TRA kutoza kodi ya Serikali kwenye sekta hii muhimu kwa Maendeleo ya Taifa letu.

Pamoja na uzinduzi huo, Serikali iliielekeza TRA na LATRA kuendelea kufanyia kazi changamoto zilizonekana ni muhimu kupewa ufafanuzi wa kina kwa wadau wa kisekta kuelekea kwenye matumizi kamili ya Mfumo huo. Kutokana na msingu huu, TRA kwa kushirikiana na LATRA, inayo heshima kubwa kukukaribisha wewe, pamoja na wadau wote wa sekta ya usafirishaji wa abiria katika Mkutano wa pamoja utakaofanyika siku ya **Ijumaa** tarehe **27 Novemba 2020** katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam kuanzia **saa nne kamili (04:00) asubuhi** kwa lengo la kujielimisha zaidi juu ya matumizi ya mfumo wa tiketi za kielektroniki, utekelezaji wake, na manufaa yake katika kukuza kipato cha wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Ewe mdau, tunakuomba upange kushiriki. Karibu sana kwenye fursa hii ili tujifunze kwa pamoja na kwa faida ya pande zote zinazohusika na kwa manufaa ya nchi yetu.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi ya urejeshaji mali za ushirika isipungue

**SERIKALI** imerejesha mali mbalimbali za vyama kadhaa vya ushirika nchini, ambazo zinadaiwa kuporwa kiujanja.

Vyama vya Ushirika vya Nyanza (NCU), Geita (GCU), Simiyu (SIMCU) na Shinyanga (SHIRECU) vimerejeshewa mali zenye thamani ya Sh. bilioni 61 zilizokuwa zikimilikiwa kinyume cha utaratibu.

Akikabidhi hati 37 kwa wenyeviti wa vyama hivyo jijini Mwanza, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema kazi hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli aliyoyatoa Agosti mwaka 2016.

Hati hizo zinahusisha ardhi, majengo na mitambo yenye thamani ya kiasi hicho cha fedha zilizoporwa kinyemela na watu kutoka vyama hivyo vya ushirika ambao ndio walikuwa wamiliki halali.

Kusaya alisema kazi hiyo ya kufuatilia na kurejesha mali imefanywa na timu maalum iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mwaka 2016 baada ya agizo la Rais Magufuli alipofanya ziara mkoani Mwanza kuwa mali zote za Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza zifuatiliwe na kurejeshwa toka kwa waliozimiliki kinyume cha utaratibu.

Kadhalika, Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (SHIRECU), kimekabidhiwa hati saba za mali za viwanja na nyumba, zilizoporwa na kuuzwa kinyume cha utaratibu.

Mwenyekiti wa timu iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, kufuatilia mali zilizoporwa za SHIRECU, Asangy Bangu, alisema juzi kuwa wamefanikiwa kurudisha viwanja saba, pamoja na nyumba ambazo ni mali za SHIRECU.

Alisema wamefanikiwa kurudisha viwanja saba vilivyopo mkoani Shinyanga, nyumba ya ghorofa tatu ambayo ipo Ilala, pamoja na ghala lililopo Kurasini jijini Dar es Salaam, ambazo ni mali za SHIRECU.

Katibu Mkuu Kusaya, aliipongeza timu hiyo kwa kufanya kazi kwa uzalendo, ambayo ilikuwa na mizengwe mingi, huku akiutaka uongozi wa SHIRECU, kuzitunza mali hizo na zisiweze kurudi tena mikononi mwa watu binafsi.

akikisha wanaushirika wananufaika na mali zao, Kusaya aliwaagiza viongozi wa vyama vya ushirika kuhakikisha mali hizo zinatumike kwa manufaa ya wakulima ambao ndio wamiliki.

Kurejeshwa lwa mali hizo ni hatua ya kupongeza kwa kuwa wizi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali ya umma vilikithiri, kiasi cha kuviacha vyama vya ushirika katika umaskini wa kutupa.

Hakika ni hatua mbele kwa kuwa miaka kadhaa iliyopita hatukushuhudia mamlaka za serikali zikichukua uamuzi huu ngumu wa kuwapa kibano waliopoteza mali za ushirika katika maeneo mbalimbali ya nchi ili wazirejeshe.

Uchunguzi wa muda mrefu ulibainisha kuwa waliohusika kufilisi mali za wanaushirika ni viongozi na watendaji, ambao baadaye walijimilikisha wenyewe na kuwaacha hoi wanachama.


Pamoja na hatua hiyo, bado kuna mali nyingine nyingi zinaendelea kuwa mikononi mwa wajanja katika maeneo mengine, hivyo kuna kila sababu ya kuendeleza kibano ili zirejeshwe kwa wenyewe.

Ni jambo lililowazi kwamba waliojimilikisha mali hizo wanafahamika, hivyo ni kazi rahisi ya kuzirejesha kwa kuwashirikisha wananchi, ambao ndio wanachama wa vyama hivyo.

Tunafahamu pia kuwa kuna kesi mbalimbali zilizoko kwenye mahakama zetu zilizofunguliwa na Jamhuri dhidi ya watuhumiwa, ambazo tunasubiri mahakama zitoe haki.

Tumaamini kwamba serikali itaendeleza kibano kuhakikisha mali hizo zinarejeshwa, ili kuwarejeshea nguvu ya kiuchumi wanaushirika. Itakumbukwa kuwa ushirika ndio tegemeo kubwa kwa maendeleo ya wakulima, wafugaji na wavuvi

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Meza ya majadiliano tiba ustawi 'bustani' demokrasia

**TANGU** kumalizika kwa uchaguzi mkuu, baadhi ya vyama vya siasa vya upinzani vimetoa matamko mbalimbali yakiwamo kuunga mkono uchaguzi huo kwamba ulikuwa huru na wa haki.

Vingine vimegoma kuutambua vikidai haukuwa huru na haki, hivyo havioni sababu ya kushirikiana na serikali, badala yake vinajiweka pembeni na kuiachia CCM.

Hata hivyo, Chama cha NCCR Mageuzi, chenyewe kinajipambanua kuwa kinaweka mbele zaidi maslahi ya taifa kwa kujali mazungumzo ya pamoja ili kuja na muafaka kuhusu uchaguzi huo.

NCCR-Mageuzi inaamini kwamba ingawa yapo madai ya 'figisufigisu' kwenye uchaguzi huo, lakini njia pekee kwa wanasiasa ni kuwekana sawa na kuwapo kwa meza ya mazungumzo, kwa ajili ya muafaka wa kitaifa.

Hivi karibuni mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia, anatoa rai hiyo mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuwa, asili ya kutatua matatizo huanzia kwenye mazungumzo na kuishia katika makubaliano ya kindugu.

Mbatia anaamini kuwa, kwa miaka 59 ya uhuru, Watanzania hawajatumia vizuri Tanzania ili wajipatie mahitaji ya msingi kwa wote na kuwa na furaha ya kweli.

Lakini, chama hicho kinakiri kwamba ni miongoni mwa vyama ambavyo kwa miaka 28 vinaimba wimbo wa kupata katiba mpya ya kubeba tume huru ya uchaguzi, na kwamba gharama zimekuwa kubwa kwa chama hicho.

Kinachoshauriwa na NCCR-Mageuzi ni sahihi, kutokana na ukweli kwamba, hata nchi zilizoendelea zinatumia njia hiyo kumaliza tofauti za kisiasa kwa manufaa ya kila mmoja.

Ni muhimu wanasiasa kutetea ama kuweka mbele taifa badala ya vyama kwa kukubaliana kukaa meza moja ya mazungumzo ili kutafuta mwafaka wa pamoja kuliko kususa tu na kukaa pembeni.

Meza ya mazungumzo itasaidia kila chama kutoa dukuduku lake na hatimaye kufikia makubaliano ambayo msingi wake ni kuendelea kumlinda 'mama Tanzania' kama anavyoshauri Mbatia.

Suala la meza ya mazungumzo limewahi kuhimizwa na Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Mstaafu Francis Mutungi, baada ya CHADEMA kutaka kufanya maandamano nchi nzima Septemba mosi, mwaka 2016.

Lengo la maandamano lilikuwa ni kupinga hatua ya serikali kukataza kufanya mikutano ya kisiasa, lakini Mutungi, akashauri kuwapo kwa kikao cha pamoja kati yake na viongozi wa vyama vya siasa kupata muafaka.

Wakati CHADEMA wakiwa wamepanga kufanya maandamano waliyoitwa, UKUTA, CCM nao kupitia Umoja wa Vijana (UVCCM), walikuwa wameomba kibali cha kufanya maandamano.

Kufuatia mvutano huo wa hatua ya upinzani kusisitiza kufanya maandamano licha ya katazo la serikali, msajili aliamua kuitisha mazungumzo ili kupata maridhiano, hali ambayo ilisaidia kuwapo kwa utulivu.

Kwa mantiki hiyo, ni wazi kwamba busara ya majadiliano ni njia sahihi kukabiliana na mizozo kama hiyo inayotokana na uchaguzi mkuu hadi baadhi ya vyama kutopeleka bungeni wabunge wa viti maalum.

Mwaka 2016, hata Spika Job Ndugai, aliwahi kuita wabunge wa upinzani katika meza ya mazungumzo baada ya kususia vikao.

Wakati akiitisha meza ya mazungumza, alisema, ili bunge lifanye kazi yake, linahitaji kuishinda changamoto iliyopo ya muhimili huo kutokuwa kitu kimoja, huku akielezea kuwa chanzo kikuu cha kusambaratika ni pamoja na "u-vyama" kuzidi na wabunge kutojali maslahi ya taifa.

Hayo ya Jaji Mutungi na Ndugai, ni machache yanayoonyesha umuhimu wa kukaa katika meza ya mazungumzo pale linapotokea jambo ambalo linaonekana halijakaa sawa.

Lakini, iwapo kila chama kitaendelea kuvutia upande wake bila kujali maslahi ya taifa, bado kutakuwapo na malalamiko yasiyofikia mwisho, ambayo huenda yangetatuliwa na meza ya mazungumzo.

Hivyo, ni vyema wanasiasa wakalipa uzito suala la kukutana katika meza ya mazungumzo ili kuwekana sawa na kumaliza sintofahamu iliyopo baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu.

## Magufuli awateua Shein, Mwakyembe

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli amemteua Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe.

Dk. Shein anachukua nafasi ya Jaji mstaafu Barnabas Samatta ambaye anamaliza muda wake.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, jana kwa vyombo vya habari, ilisema pia, Rais Magufuli amemteua Dk. Harrison Mwakyembe kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Taarifa hiyo ilisema Dk. Mwakyembe anachukua nafasi ya Mariam Mwaffisi ambaye amemaliza muda wake. Vile vile, Rais Magufuli amemteua Gaudensia Kabaka kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Kabaka anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili baada ya kipindi cha kwanza kumalizika.

## Pemba wapata mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIKA azma yake ya kuhakikisha huduma za mawasiliano zinakuwa za uhakika, Kampuni ya Zantel imesogeza huduma zake kisiwa cha Pemba kuwarahisha wananchi wa huko huduma kwa urahisi zaidi.

Kampuni hiyo imeamua kufungua duka kisiwani Pemba likiwa na kituo cha huduma kwa wateja kilichoboreshwa zaidi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa duka hilo, Mkuu wa Masoko na Huduma za Kifedha wa Zantel, Sakyi Opoku, alisema uwepo wa duka hilo utapunguza adha mbalimbali ambazo wateja walikumbana nazo awali.

"Uboreshaji wa duka hili ni sehemu ya mkakati wa kampuni yetu wa kuhakikisha tunasogeza huduma karibu na wateja, ili kuhakikisha wanazipata huduma na bidhaa zetu kwa urahisi zaidi," alisema.

Aidha, alisema duka hilo linatarajia kuhudumia zaidi ya wateja 100 likitoa huduma mbalimbali ikiwamo usajili wa simu, huduma za kifedha (Ezypesa) pamoja na uuzaji wa simu mbalimbali zenye uwezo wa 4G ikiwamo simu aina ya Smarta.

# Wahukumiwa faini kwa kutumia mtandao kilaghai

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu Baraka Mtunga na Rajabu Katunda kulipa faini ya Sh. milioni tatu au kwenda jela miaka miwili na kulipa fidia ya Sh. milioni 267.6 baada ya kukutwa na hatia ya makosa ya kutumia mtandao kilaghai.

Kadhalika washtakiwa hao wanadaiwa kuisababishia hasara Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya Sh. 267,656,794.30.

Pia, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Kassian Matembele, iliagiza vifaa vya mawasiliano walivyokamatwa navyo washtakiwa vinataifishwe zikiwamo simu mbili na kompyuta mpakato kuwa mali ya serikali.

Hakimu alisema mahakama yake imefikia uamuzi huo baada ya washtakiwa kuingia makubaliano ya kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano kati ya washtakiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Akisoma hati ya makubaliano, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai baada ya pande mbili kukaa na kukubaliana washtakiwa walitakiwa kulipa fidia ya Sh. 267,656,794.30 na walilipa Sh. 200,000,000.

Aliendelea kudai kuwa makubaliano hayo pia yaliwataka washtakiwa hao kumalizia kiasi kilichobaki ndani ya miezi sita. Akisoma maelezo ya awali katika kesi hiyo wakili Simon alidai, washtakiwa hao kupitia kampuni ya Uhuru One, ambayo ilikuwa haijasajiliwa kisheria walitenda makosa ya kutumia na kusambaza huduma za intaneti kwa njia ya kilaghai bila leseni.

Alidai baada ya taarifa za uchunguzi kuwafikia Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa ambao walikiri kusimika vifaa vya mawasiliano na kutumia huduma za intaneti isivyo halali.

Pia alidai kuwa baada ya uchunguzi zaidi iligundulika kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati Desemba 13, 2019 na Septemba 28, 2020.

Baada ya kusomewa maelezo hayo Hakimu Matembele aliwasomea hukumu na kuwaeleza kuwa kwa makubaliano waliyowekeana na DPP na kukiri kwao nafasi ya rufani imefungwa.

"Nafasi ya rufani inatolewa tu kwa hukumu iliyotolewa baada ya kutiwa hatiani kwa kusikilizwa ushahidi, lakini kwe vile nyie mmekiri baada ya makubaliano hakuna nafasi ya dhamana," alisema Hakimu Matembele.

Awali, washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na makosa sita ikiwamo utakatishaji fedha, makosa manne yalifutwa na kusomewa hati moja ya mashtaka yenye makosa mawili ya kutumia mtandao kilaghai na kusababisha hasara kwa TCRA.




Meneja Uhusiano wa Tecno Tanzania, Eric Mkomoya (kulia), akionyesha simu mpya aina ya Tecno Camon 16s iliyozinduliwa jana, ambayo itapatikana kwa bei nafuu kwenye maduka yote ya Vodacom nchini, ikiwa na GB 96, ni sehemu ya kuwapatia wateja punguzo katika msimu huu wa sikukuu. Kushoto ni Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania PLC, George Lugata. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Amref, wasanii waadhimisha wiki ya usafi mazingira

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Amref Health Africa Tanzania na wasanii wa kizazi kipya Zena Mohamed 'Shilole' na Balozi wa kampeni ya Nyumba ni Choo, Mrisho Mpoto (pichani), wameungana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuadhimisha wiki ya usafi wa mazingira kwa kufanya uhamasishaji wa usafi wa mazingira na kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka katika shule 19 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo kilichofanyika Buguruni, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng`wilabuzu Ludigija, aliipongeza Amref kwa kuweka kipaumbele suala la usafi wa mazingira.

"Usafi wa mazingira ni muhimu hasa kwa watoto wetu wakiwa shuleni na maeneo yenye msongamano kama masoko. Nitoe rai kwa wananchi kuendelea kuzingatia tabia ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni ili tuwe salama," alisema Ludigija.

Alisema katika Manispaa ya Ilala, wamepata mafanikio makubwa ya kampeni ya usafi wa mazingira kwa kuwa mwaka wa nne sasa hawajasikia magonjwa ya mlipuko.

Meneja Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira wa Amref Tanzania, Mturi James, alisema wataendelea kushirikiana na serikali kuleta mabadiliko ya kudumu katika sekta hiyo.



Alisema lengo ni kuchangia juhudi za serikali kutekeleza miradi ya kuboresha huduma za afya na maendeleo ya jamii kupitia sera na miongozo ya afya ya kitaifa.

"Tunafanya miradi yote hii, ili kujibu vipaumbele vya afya vya kitaifa na malengo ya maendeleo endelevu katika kushughulikia mahitaji ya afya ya wanawake na watoto," alisema James.

"Tunajitahidi kuongeza ufanisi na uendelevu wa huduma hizi kwa kuchangia na kuimarisha mifumo ya afya, kuboresha upatikanaji wa huduma na kuhamasisha mifumo ya afya ya jamii na sera kwa ujumla."

Kwa upande wake msanii wa kizazi kipya, Shilole alisema wamekuwa wakizunguka katika shule mbalimbali kujenga hamasa ya umuhimu wa usafi wa mazingira.

Wiki ya usafi wa mazingira mwaka huu imebebwa na ujumbe wa "Mahitaji ya jinsia kwa mazingira endelevu" ikihamasisha jamii kuzingatia mahita ya jinsia katika utoaji wa huduma za usafi wa mazingira.

# TARI yajipanga kuakisi maono ya Magufuli mazao ya mkakati

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

BODI ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imewataka watafiti wake kuongeza kasi katika kuleta mapinduzi ya kilimo ili kuongeza malighafi ya kutosha kwenye ukuaji wa viwanda vya ndani.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Yohana Budeba, aliyasema hayo eneo la Masigati, wilayani Manyoni mwishoni mwa wiki, unaotekeleza mradi wa 'Kilimo cha Pamoja' cha korosho, alipotembelea na kuangalia sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya bodi kwa taasisi yake.

Mbali na kupongeza dhamiri ya dhati ya Rais John Magufuli katika kuinua tija ya kilimo nchini kupitia hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge la 12, aliwataka watafiti na wadau wengine wa kilimo kuunga mkono juhudi za serikali, ili kuchagiza kasi ya mabadiliko hayo, sambamba na kusukuma ukuaji wa uchumi.

Alisema katika kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo na maelekezo ya serikali, bodi yake imefarijika kuona maagizo iliyotoa kuhakikisha ugunduzi na teknolojia zote zinawafikia walengwa, limezingatiwa na kutekelezwa kikamilifu.

Baadhi ya maagizo yaliyotolewa na bodi hiyo ni kuitaka TARI kusambaza kwa kasi teknolojia zake hususani eneo la ugunduzi wa mbegu bora jambo ambalo limeendelea kutekelezwa.

Agizo lingine ni kuitaka TARI kufanya utafiti wenye lengo la kupanua wigo wa kilimo cha korosho kutoka mikoa mitano iliyokuwa ikizalisha jambo ambalo nalo limetekelezwa ipasavyo.

Katika kutekeleza hilo, TARI imebainisha mikoa 20 yenye uwezo wa kuzalisha korosho, ikiwamo Singida katika eneo la Msigati ambalo limeanza uzalishaji katika ekari 22,000. Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema hitaji la taasisi hiyo kwa sasa ni kuona uzalishaji wa teknolojia zake, ubunifu na mbinu bora za kilimo zinakwenda sambamba na ukuaji wa viwanda.

Alisema malengo ya taasisi ni kuongeza juhudi katika kuhakikisha kiwango cha asilimia 60 za malighafi ya kilimo zinapatikana kwenye viwanda vya ndani.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wapili kulia) na Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Rasuli Masudi (wapili kushoto), wakizindua rasmi kampeni ya Mastabata 2020 jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Kadi NMB, Philbert Casmir na Meneja Mwandamizi wa Kadi, Manfred Kayala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yahamasisha matumizi ya kadi

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya NMB imeanzisha kampeni maalum iitwayo MastaBata yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya kadi kwenye manunuzi badala ya fedha taslimu ambayo yanatajwa kuwa si salama kwa kuwa kuna wakati huchochea uhalifu.

Hatua hiyo inatajwa kuwa inaunga mkono juhudi ambazo pia zinafanywa Serikali ambayo imeendelea kuboresha mfumo wa malipo mengi kwa kuhakikisha hayafanywi kwa fedha taslimu badala yake yanalipiwa kwa mfumo maalumu ikiwamo kadi na simu za mkononi.

Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi na Menejiment ya NMB, kwenye uzinduzi huo Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, alisema NMB imeamua kutoa fursa ya kipekee kwa wateja wake kufurahia huduma za benki hiyo kupitia promotion hiyo ambayo itatoa zawadi hizo zenye jumla ya Sh. milioni 200.

Kupitia promosheni hiyo itakayoendeshwa kwa miezi mitatu, NMB inalenga kutumia na wateja wake faida waliyoipata, hivyo zawadi mbalimbali zitatolewa, ikiwamo mshindi kuambatana na mwenzi wake kwenda kufanya utalii wa ndani Zanzibar au kwenye mbuga za wanyama Serengeti na Ngorongoro.

"Kampeni itakuwa na droo za kila wiki na kila mwezi, wateja wanapaswa kufanya miamala yao kupitia kadi ya NMB Mastercard au QR mara nyingi iwezekanavyo kwa kuwa unapofanya muamala unaongeza nafasi moja ya kushinda," alisema.

Mponzi alibainisha pia kadri mteja anavyotumia kadi katika ununuzi kwenye mtandao au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS)katika maduka mbalimbali ndivyo unavyopata nafasi nzuri zaidi ya kushinda.

Kwa mujibu wa Mponzi, katika kipindi chote za kampeni hiyo MasterBara 'siyo ki kawaida' wanatarajia kupata washindi 40 wa fedha taslimu 100,000 kila wiki na washindi 15 wa simu janja aina ya Samsung galax note20 yenye thamani ya Sh. 2,480,000 au jokofu na runinga kila mwezi.

Alisema hata hivyo, wameweka nafasi kwa washindi wa utalii wa ndani iwapo hawatakuwa tayari kwenda kutalii wanaweza kubadilisha zawadi kwa kuchukua runinga ya kibabe iliyolipiwa na DSTV miezi mitatu au jokofu la milango miwili, kompyuta mpakato, water dispenser na microwave .

Kampeni hiyo iliyoanza rasmi jana, inatarajiwa kufikia kilele chake Februari 21, wateja wote wakiwamo watakaojiunga katika kipindi hiki baada ya promosheni kuanza wanaruhusiwa kushiriki.

Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Rasuli Masudi, alihamasisha wateja na wananchi wengine kujiunga kushiriki kwenye promosheni hiyo kwa kuwa imethibitika kuwa ni halali inazingatia vigezo vyote vya utoaji wa zawadi kwa watakaoshinda.

# Uhamasishaji shirikishi chakula wapamba moto

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, amesema uhamasishaji upatikanaji chakula shuleni unafanyika kwa kushirikiana na wazazi ili kuhakikisha watoto wanapata utulivu husuani muda wa masomo.

Ntemo amesema uhamasishaji huo wa watoto kupata chakula, mbali na utulivu, pia unalenga kupunguza utapiamlo hususani wa ukondefu kwa wanafunzi.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kuhusiana na mikakati waliyojiwekea kutokomeza udumavu ikiwa ni baada ya wakuu wa wilaya kutia saini mkataba wa lishe na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo.

Ntemo alisema kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, shule 20 kati ya 43 za msingi na za awali zinatoa chakula (uji) kwa watoto muda wa mapumziko.

Pia alibainisha kuwa upande wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, shule za serikali tatu zenye mahitaji maalumu wanafunzi wanapata chakula cha mchana wakiwa shuleni.

Aidha, alisema shule za msingi 26 za binafsi kati ya 62 zilizopo (serikali na binafsi), wanafunzi wanapata chakula cha mchana kwa madarasa ya awali na ya mtihani na kwamba chakula kinachotolewa ni ugali, wali, maharage, mboga za majani na uji wa mchele.

Kuhusu elimu ya sekondari, wataalamu wa lishe wanaendelea kufanya usimamizi shirikishi katika shule za bweni na hosteli na kuangalia utoaji wa lishe bora kwa wanafunzi.

"Wilaya ya Kibaha inaahidi kuendelea kusimamia utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kutenga fedha za kutekeleza afua za lishe kupunguza utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano, kupunguza hali ya ulemavu," alisema.

Alipongeza kuwa wilaya hiyo inaendelea kuhakikisha wazazi wananyonyesha watoto wao maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo na wajawazito kupewa vidonge vya kuongeza damu.

Mmoja wa wakazi wa Maili Moja, Abeda Juma, alishauri huduma ya chakula iwapo na kwamba wazazi washirikishwe kwenye vikao kwa kuwa fedha wanazowapa watoto wanapokwenda shuleni kila siku ni nyingi kulinganisha na kipato walicho nacho.

"Niko tayari kuchangia watoto wapate chakula shuleni ninachoomba uchangiaji uwe wa kiwango ambacho kila mwananchi atamudu kuchangia kwani huduma hiyo ni jambo nzuri. Watatuokoa kuwapa fedha za kutumia shuleni, naomba hili lifanyike kwa vitendo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Sababu kuifanya Hifadhi Nyerere bora duniani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI inakusudia kuifanya Hifadhi mpya ya Taifa ya Nyerere iliyomegwa kutoka Pori la Akiba la Selous lililopo mkoani Morogoro, kuingia katika hifadhi bora duniani kutokana na kuwapo kwa wanyama na viumbe hai ambao wengine hawapatikani sehemu nyingine.

Hatua hiyo inatokana na hifadhi hiyo kabla ya kukabidhiwa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) wakati ikiwa Pori la Akiba la Selous kuwa katika tishio la kupoteza sifa za uhifadhi kutokana na vitendo vya ujangili.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Allan Kijazi, wakati akifunga mafunzo ya awali kwa askari 561 wa Jeshi la Uhifadhi na Misitu yaliyofanyika eneo la Matambwe katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere mkoani Morogoro.

**Kabla haijatangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, hili eneo lilikuwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous, hivyo kulikuwa na tishio la kupoteza sifa za uhifadhi duniani kutokana na majangili kushambulia sana tembo na wanyama wengine.**

Dk. Kijazi ambaye ni Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, alisema maamuzi ya kuifanya hifadhi hiyo kuwa bora inachangiwa na kuwapo kwa mradi wa ufuaji umeme kwa kutumia maji wa Nyerere ambao upo ndani ya hifadhi hiyo, hivyo kuwa moja ya kivutio kikubwa cha wageni kutembelea.

"Kabla haijatangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, hili eneo lilikuwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous, hivyo kulikuwa na tishio la kupoteza sifa za uhifadhi duniani kutokana na majangili kushambulia sana tembo na wanyama wengine," alisema na kuendelea:

"Sasa tumejipanga kuhakikisha inakuwa hifadhi bora duniani kuliko zote za nchini."

Alisema kutokana na umuhimu huo, ndio maana TANAPA imeamua kuendesha mafunzo ya awali ya Jeshi la Uhifadhi kwa ajili ya askari wapya ambao watafanya kazi ndani ya hifadhi hiyo mpya.

Aliwataka askari hao kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama za wilaya zinazozunguka hifadhi hiyo kutengeneza mkakati maalumu wa kiulinzi ili kukabiliana na ujangili.

Naye Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA Kanda ya Mashariki, Asteria Ndaga, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo, ujasiri, uzalendo na uadilifu wa usimamizi wa rasilimali za wanyama na misitu kwa faida ya Watanzania.

Alisema kuwa mafunzo hayo yamefanyika kwenye maeneo tofauti yenye wanyama wakali, milima na mabonde na misitu kwa lengo la kuwapa ujasiri na uvumilivu askari huo wanapokuwa kwenye kazi zao.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, ambaye wilaya hiyo imezunguka hifadhi hiyo, alisema watatoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha wanaimarisha ulinzi ndani na nje ya hifadhi hiyo.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa, akionyesha jana kwa waandishi wa habari baadhi ya vitu vinavyodhaniwa kuwa vya wizi, ambavyo watu waliokuwa wamevipakia katika pikipiki waliviacha na kutoroka. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanafunzi waaswa matumizi ya simu

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWENYEKITI mstaafu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Nawab Mullah, amewataka wanafunzi kuepuka matumizi ya simu za mkononi kwani zimekuwa chanzo kikubwa cha kuwapotosha na kujiingiza katika matendo yasiyo na maadili.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali katika Shule ya Sekondari ya Kawe Ukwamani, jijini Dar es Salaam, alisema wanafunzi wanapoteza muda mwingi kutazama video za ovyo au za wanamuziki na tamthilia tu.

Mullah ambaye ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Afritea Tanzania Tea Blenders, alisema, atafanya mchakato wa kuratibu namna ambavyo watoto hasa wanaotoka katika familia zenye vipato duni na yatima, wasaidiwe kupata chakula.

Aliwaomba wazazi wenye uwezo ambao wana wanafunzi katika shule hiyo kujaribu kutengeneza mpango wa kuchangishana fedha walau kiasi kidogo kidogo, ili kuokoa hatima ya watoto hao ambao wanatoka katika familia zisizo na uwezo.

Uongozi wa shule hiyo ulieleza kuwa shule inakabiliwa na ukosefu wa kompyuta na mashine ya kurudufia (photocopy), vyoo kujaa maji kutokana na eneo la shule kuwa oevu na uhaba wa chakula kwa ajili ya wanafunzi hasa wanaotoka katika familia zenye kipato duni na yatima.

"Mimi ni Mwenyekiti mstaafu wa CCM Mkoa wa Mbeya, na nilikuwa nagombea kuteuliwa na CCM ili nigombee ubunge Jimbo hili la Kawe, sasa msidhani kukosa kwangu ubunge kutanifanya niache kuyatekeleza yale yote niliyokuwa nimekusudia kuwafanyia wananchi wa Kawe kama ningeupata ubunge," alisema Mullah.

Mullah pia aliahidi kuangalia namna atakavyoweza kusaidia kukabili vikwazo vinavyoikabili shule hiyo.

**...Sasa msidhani kukosa kwangu ubunge kutanifanya niache kuyatekeleza yale yote niliyokuwa nimekusudia kuwafanyia wananchi wa Kawe kama ningeupata ubunge.**

# DC ashangazwa zahanati kuwa na muuguzi mmoja

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, amemwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Morogoro kumrejesha kazini mara moja daktari wa zahanati ya Msonge iliyopo Halmashauri ya Morogoro ambaye ameenda likizo zaidi ya wiki mbili na kuacha zahanati ikiwa na muuguzi mmoja.

Kutokana na hali hiyo, muuguzi huyo analazimika kuhudumia idadi kubwa ya wagonjwa.

Msulwa alitoa agizo hilo baada ya kukuta muuguzi huyo akiwa amezidiwa na wagonjwa, ambapo alisema jambo hilo haliwezi kuvumilika, kwani linahatarisha maisha ya watu kwa kukosa huduma bora za afya.

Alisema serikali imejipambanua kwa kuwasaidia wananchi wa chini kupata huduma bora za kijamii ikiwamo huduma ya afya, hivyo daktari huyo anapaswa kurejea kazini ili kusaidia wananchi.

"Nimekuta huyu muuguzi hapa anafanya kazi zote kuanzia kupokea wagonjwa kupima na kuwahudumia bila kupumzika... hili ni jambo la hatari sana licha ya kwamba anaokoa maisha ya watu kisa daktari ameenda likizo, hii haiwezekani, lazima mganga mkuu wilaya DMO aje hapa na amrejeshe huyu daktari," alisema Msulwa.

Theresia Ndambaru, muuguzi pekee katika zahanati hiyo, alikiri kuzidiwa na wagonjwa baada ya kukosa usaidizi katika kutoa huduma na kuiomba serikali kuchukua jitihada za haraka kuongeza wahudumu wa afya kwenye zahanati hiyo.

Alisema miongoni mwa vikwazo vikubwa ni pale inapotokea kuwapo kwa mzazi anayetaka kujifungua, ambaye anahitaji uangalizi wa karibu na wakati huo huo kunakuwa na wagonjwa wengine wanasubiri huduma, jambo linalomfanya kushindwa kijigawa kutoa huduma.

"Sina muda wa kupumzika kwa sababu usiku nilikuwa na mzazi anajifungua, ambaye anahitaji msaada na baada ya muda akaletwa mtoto ambaye amezidiwa, nilijitahidi kumuhudumia lakini ukweli ni kwamba nafanyakazi katika mazingira magumu kwa sababu daktari wangu hayupo, ameenda likizo," alisema Theresia.

Akizungumzia hatua watakazozichukua kwa haraka kutatua kikwazo hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Patrick Mwakiriri, alisema suala lililotokea la dakatari huyo kwenda likizo ni la dharura, hivyo halmashauri itafanya jitihada za makusudi kwa kumhamisha daktari mmoja kutoka Kituo cha Afya Mvuha ili kuziba nafasi ya daktari huyo.

# Wachimbaji waomba huduma ya majisafi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WACHIMBAJI wadogo katika mgodi wa Kabela Gold Mine katika Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Kahama Mjini, wameiomba serikali kwa kushirikiana na uongozi wa mgodi huo kuwapelekea huduma ya majisafi na salama ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji.

Waliyabainisha hayo wakati wakizungumza na vyombo vya habari kwa nyakati tofauti vilivyofika mgodini hapo, kuangalia namna shughuli za uchimbaji na uzalishaji wa madini unavyoendelea, na uongozi unavyoshiriki katika kupeleka huduma za maendeleo katika vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

Lameck Japani, katika mgodi kuna ukosefu huduma ya maji ya uhakika na kusababisha kununua dumu moja la lita 20 kwa Sh. 1,000 hadi 1,500 kwa ajili ya kuoshea mawe yanayosadikika kuwa na madini.

**Kwa sasa huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) yameshafika Kata ya Zongomela na kilichobaki ni ulazaji wa mabomba ya maji na kufika katika maeneo ya mgodi.**

Alisema kabla ya kupelekewa huduma ya nishati ya umeme pia walikuwa wakitumia gharama kubwa (majenereta) katika uendeshaji wa mgodi hasa wakati wa kuvuta maji ndani ya madura ya kuchimbia dhahabu, lakini baada TANESCO kuwafungulia huduma hiyo, gharama zilipungua.

Naye Yusta Kisuma, alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenye uendeshaji hasa wakati wa kuosha mawe yanayosadikika kuwa na dhahabu kwa kutumia maji mengi, ambayo upatikanaji wake ni shida, lakini mwisho wa siku wamekuwa wakipata ujira kidogo ukilinganisha na kile walichotumia.

Mwenyekiti wa mgodi huo, Joseph Nalemi, alithibitisha kuwapo kwa ukosefu wa huduma ya maji ya kutosha na kwamba kila siku amekuwa akitoa shilingi 20,000 kwa ajili ya kuchota maji ambayo yanatumika kwenye vyoo ndani ya mgodi, ili kuviweka katika hali ya usafi na kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Alisema kwa sasa huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) yameshafika Kata ya Zongomela na kilichobaki ni ulazaji wa mabomba ya maji na kufika katika maeneo ya mgodi.

Hata hivyo, Nalemi aliwataka KUWASA kuangalia namna ya kuyafikisha maji kwenye eneo la mgodi ili kuongeza kasi ya uzalishaji na uchumi wa kila mchimbaji na kulipa kodi za serikali kwa wakati, kwa kuwa na uzalishaji utaongezeka na fedha zitapatikana kwa urahisi.



Ofisa Kilimo wa Kata ya Mondo, Halmashauri ya Kishapu mkoani Shinyanga, Pius Maganga (kulia), jana akitoa elimu ya namna ya kulima bustani ya viazi lishe katika moja ya bustani za lishe inayopo kijiji cha Wishiteleja kwa wananchi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wakazi Kisiju wamwomba JPM gati

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAKAZI wa Kisiju Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wamemwomba Rais John Magufuli, kuwatatulia kero yao sugu ya ujenzi wa gati.

Wakizungumza na Nipashe, kijijini hapo kwa nyakati tofauti, wakazi hao, walisema kuwa kuwapo kwa gati kutawasaidia kufanya kazi zao katika mazingira mazuri.

Diwani wa Kata ya Kisiju, Ally Day, aliiambia Nipashe kuwa wanamwomba Rais Magufuli awatengenezee gati, ikiwamo na kurasimisha bandari yao ili iweze kuwainua wananchi, ambao asilimia kubwa ni wavuvi.

"Umuhimu wa gati unasaidia wananchi na watumishi katika vijiji vya Koma, Kwale, Kuruti na Kisiju ambavyo vimezungukwa na Bahari ya Hindi, hivyo mahitaji yao muhimu lazima waje Kisiju Pwani," alisema Day.



Aliongeza kuwa abiria ambao wanatumia usafiri wa jahazi kutoka Mafia kuelekea Dar es Salaam ni rahisi kupitia Kisiju kama zamani badala ya Nyamisati.

Alisema kwa kufanya hivyo, kutachochea wananchi kuboreka kiuchumi ikiwamo serikali ngazi ya kijiji, kata na halmashauri ya wilaya na Serikali Kuu kutopoteza mapato yake.

Pia, alimwomba Rais Magufuli, kuwakumbuka barabara yao ya Mkuranga Kisiju kwa kuwawekea lami, kama alivyoahidi na kwamba hali hiyo itasaidia kupanua uchumi wa wilaya.

# Diageo yaunga mkono maendeleo endelevu

**Na Mwandishi Wetu**

DIAGEO, kampuni mama ya Bia ya Serengeti (SBL), imetangaza mpango madhubuti wa miaka 10 unaolenga kutoa mchango chanya kwa maendeleo duniani kufikia mwaka 2030 ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Umoja wa Mataifa kupitia mpango wake wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Hayo yamebainishwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Diageo, Ivan Menezes na kubainisha kuwa kupitia mpango huo wa miaka 10, Diageo itajikita katika sehemu kuu tatu ambazo zimechaguliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa.

Alisema sehemu hizo ni kuhamasisha unywaji wa kistarabu, kuhakikisha ushirikishwa wa jamii katika shughuli mbalimbali, pamoja na kuhamasisha kilimo endelevu.

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, SBL inayomilikiwa na Diageo, imekuwa ikiendesha kampeni ya kuhamasisha unywaji wa kistarabu kupitia kampeni ya kitaifa ya "Usinywe na kuendesha chombo cha moto" ikishirikiana na wadau mbalimbali kama Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani. Kampeni hii imeweza kuwafikia zaidi ya watu 100,000 wakiwamo madereva bodaboda, madereva wa mabasi na umma kwa ujumla.

Katika kilimo endelevu, SBL inafanya kazi na mtandao wa wakulima 400 wanaolima mazao kama mahindi, mtama na shayiri ambao kwa sasa wanasaidia kuipatia kampuni asilimia 80 ya malighafi inayohitaji katika uzalishaji wa bia zake kwa mwaka.

Kupitia programu yake ya Kilimo Viwanda, kampuni inatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo ikilenga kusaidia kuongeza wataalamu wa kilimo nchini ambao ni nguzo muhimu katika maendeleo ya sekta hii mama.

Kwenye ushirikishi wa jamii, imechimba visima 17 katika maeneo mbalimbali hapa nchini yenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma ya maji, hivyo kuwezesha jamii na haswa kinamama na watoto wa kike ambao hubeba mzigo wa kutafuta maji kuweza kunufaika na huduma ya majisafi na salama karibu na maeneo yao.

Kadhalika, inatoa likizo ya uzazi kwa miezi sita ikiwa ni zaidi ya ile ya miezi mitatu inayotakiwa kutolewa kisheria.

Akizungumzia kuhusu mpango huo, Menezes, alisema: "Tukiwa kama wadau wa biashara duniani, tunao wajibu wa kulinda dunia yetu na kuifanya kuwa sehemu salama ya kuishi kwetu sisi na vizazi vijavyo. Ninayofuraha kubwa kwa mchango wa maendeleo ambao Diageo imeweza kuutoa kufikia leo. Mpango huu mpya utatuwezesha kuendelea kutoa mchango mkubwa zaidi kufikia 2030.

# ‘Lissu alipopangua umuhimu wa ‘kigogo’ uchaguzi mkuu’

Ukurasa 12





Ukurasa 14

**KIJANA BOBI WINE**

siasa
JUMATANO NOVEMBA 25, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

UCHAMBUZI

# Uvumilivu kisiasa una umuhimu harakati za kutanzua mkwamo

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI mkuu wa mwaka 2020 umemalizika kwa kutumia katiba iliyopo ya 1977 ambayo ndiyo inayounda na kuipa uhalali Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuratibu na kusimamia mchakato wa uchaguzi.

Baada ya uchaguzi huo, vyama vya upinzani vikiwamo CHADEMA na ACT-Wazalendo vimesusia na kusisitiza kuwa haviko tayari kutambua matokeo, na havitapeleka wabunge hasa wa viti maalumu bungeni licha ya kwamba havina wa majimbo.

Aidha, Mwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahimu Lipumba, anatangaza kuwa hatakuwa tayari kushiriki uchaguzi mkuu wowote, na kwamba kipaumbele chake ni ulazima wa kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Yote hayo yanaashiria kuwa na madukuduku na mkwamo wa kisiasa ambao unawagusa wapinzani, wapigakura, serikali, wadau wa uchaguzi wa ndani na nje na NEC.

Ikumbukwe uchaguzi ni mchakato unaohusisha wadau wengi kuanzia wagombea, wapigakura, vyama, NEC, mahakama, vyombo vya ulinzi na usalama, asasi za kiraia, Umoja wa Afrika na waangalizi wa nje na ndani.

Na kwa mujibu wa ibara ya 74 ya katiba ya Tanzania ya 1977, NEC ndiyo inayosimamia na kuratibu masuala yote ya uchaguzi, hivyo baadhi ya kasoro za uchaguzi zinazohusiana na tume hiyo zitapatiwa majibu iwapo kutafanyika marekebisho ya katiba na kupatikana tume mpya.

Wakati ule wa kuanzisha mchakato wa kutafuta maoni ya wananchi kuhusu katiba mpya, hadidu za rejea za Tume ya Jaji Joseph Wariba iliyochukua jukumu la kuwafikia Watanzania na kusikia maoni yao, zilielekeza kupatikana kwa katiba mpya mwaka 2014 ili itumike kwenye uchaguzi mkuu wa 2015. Hata hivyo,



Profesa Ibrahim Lipumba, mgombea wa urais wa CUF 2020 , ambaye ametangaza kusimamia kidete uwepo wa tume huru ya uchaguzi. **PICHA: MTANDAO.**

haikuwezekana na hilo limeendelea kuwa kasoro kila baada ya uchaguzi mkuu tangu ule wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi uliofanyika mwaka 1995.

Wakati michakato ya kuunda baraza la mawaziri ikiendelea na matayarisho ya vikao vya bunge la awamu ya pili litakaloongoza kuanzia 2020 hadi 2025, ni vyema wadau hasa wanasiasa wapinzani wakaendeleza utamaduni wa kuwa na uvumilivu wa kisiasa (political tolerance) na kufanya majadiliano na serikali kuhusu uwezekano wa katiba mpya itakayoleta NEC mpya.

Uvumilivu wa kisiasa ndiyo utakaowezesha kila upande kumthamini mwenzake bila kujali kuwa ni sehemu ya bunge au diwani ama hakuchaguliwa na wananchi kuwawakilisha au yeye hana cha kuleta kwa serikali iliyoko madarakani.

Kwa maana nyingine ni kwamba, chama ama mdau huyo wa kisiasa hawezi kusikilizwa kwa maana hajapewa nafasi ya kuwakilisha wananchi iwe jimboni au kwenye kata.

Uvumilivu wa kisiasa ndiyo unaowezesha vyama tawala na mahasimu wake (upinzani) kukubali kuwa kila upande una nafasi katika demokrasia, kadhalika kupeana nafasi ya kuwajibika kwa umma kwa maelekezo ya katiba na sheria.

Pendekezo la Profesa Lipumba kuwa ataachana na uchaguzi kwanza kushinikiza katiba mpya, huenda halina tija kidemokrasia, kwa kuwa ni ajenda ambayo alianza kuizungumzia muda mrefu na haijawa na mafanikio, hivyo aendelee kuwa na uvumilivu wa kisiasa hadi mambo yatakapotengemaa, lakini si kukimbia uchaguzi.

Kuna mambo mengine ambayo yamekuwa yakizungumzwa na wapinzani ikiwa ni pamoja na kufikishwa na kupingwa mahakamani matokeo yote ya uchaguzi bila kujali iwe ni wabunge, madiwani na rais. Yote haya hayajafanyika, lakini ni vyema upinzani ukaendelea kuyasisitiza wakati huo ukiendeleza uvumilivu huo.

Kwa mujibu wa katiba ya 1977 matokeo ya urais yakishatangazwa hayawezi kupingwa popote.

Lakini pia, lipo suala la mgombea huru au binafsi ambalo nalo limekuwa miongoni mwa ajenda zinazozungumzwa na wapinzani na wadau wanaofuatilia masuala ya demokrasia.

Yote hayo katiba ya sasa haiyaruhusu kwa mfano, inaeleza jinsi ya kupata mgombea wa ubunge, udiwani au urais ikifafanuliwa ndani ya sheria ya uchaguzi mkuu ya mwaka 2010 kuwa ni lazima yeyote atokane na chama, ndiyo maana ili kufanikisha ni lazima pande zote za kisiasa iwe serikali ama wapinzani waendeleze uvumilivu wa kisiasa na kuyatafutia ufumbuzi.

**KUUNDA NEC MPYA**

Katiba ni chombo cha nchi na si mali ya mtu au kikundi, ndiyo maana rasimu ya Warioba ilitolewa ili wananchi watoe maoni yao na wapinzani walidai kuwa walipoona kuwa hawakuridhika walipinga na kutoa msimamo dhidi yake baada ya kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Kama ilivyokuwa kwa rasimu ambayo ilitolewa ili Watanzania waisome, waielewe, watoe ushauri waongeze yale ambayo hayapo wapendekeze hoja za kuondoa pengine ni vyema wakaangalia na NEC na kupendekeza kile ambacho wanataka kiwepo.

Kuanza kutoa lawama kwenye NEC wakati hakuna marekebisho yaliyofanywa kwenye katiba hakuna tija, hivyo si wakati muafaka kuwaambia Watanzania kuwa chama kitasusia uchaguzi hadi kuwe na tume mpya ni vyema kuanza majadiliano ya kuanzisha mchakato wa kupata maoni ya NEC mpya ili kipatikane kile wanachotaka kisimamie uchaguzi na kiwe ndani ya katiba.

Uchaguzi ni suala la kikatiba sio la chama fulani kusema hakiutaki. Ikumbukwe chama kinaweza kuondoka madarakani, lakini katiba na NEC vikadumu. Mfano Zambia chama cha mwasisi Kenneth Kaunda cha UNIP, Kenya KANU iliyoanzishwa na Baba wa Taifa Jomo Kenyatta na cha Malawi Congress Party vyote vimekufa, lakini katiba na mataifa hayo vinaendelea kuwapo.

Uvumilivu wa kisiasa ndiyo utakaofanikisha michakato ya katiba mpya yenye NEC mpya.

Akizindua bunge mapema mwezi huu Rais John Magufuli, anasema serikali itaudumisha muungano na utadumu na utaendelea kuwa thabiti na kuwepo na kwamba nia ya Tanzania na Zanzibar kuudumisha.

Kwa hiyo hilo nalo pamoja na tume ya uchaguzi ni hoja ya kuzichukulia kikatiba na kuziwekea vipengele vinavyosisitiza umuhimu wa kulinda na kuhifadhi muungano.

Kuna baadhi ya mambo yanayotishia kuvunja muungano ambayo iwapo yatawekwa sawa kwenye katiba mpya, hakuna atakayesimama na kuikanusha ili kuendeleza nia thabiti ya kulinda na kuutetea.

# ‘Lissu alipopangua umuhimu wa ‘kigogo’ uchaguzi mkuu’

**Na Ani Jozeni**

KUNA usemi kuwa historia hujirudia, ila mhenga mmoja aliyesoma busara hiyo alishangaa kuona kuwa tukio la kihistoria halijirudii kwa njia ile ile bali linaonyesha utofauti kimantiki.

Anagundua, mhakiki semi huyo anapoona kuwa ni kweli watu mashuhuri hutokea kana kwamba ni mara mbili katika historia, ila kwanza inakuwa mkasa yaani jambo la kushtusha na kushangaza na mara ya pili inakuwa kama mzaha kitu ambacho kinashangaza, ila hakina mantiki.

Ukiangalia matukio ya ‘mduara’ wa uchaguzi nchini kuna taswira kama hiyo inajitokeza; katika sura nyingine.

Wakati wa kuhamia upinzani kwa Edward Lowassa, mwaka 2015, kulitokea kama mkasa, kwa sababu umoja wa makada uliotayarisha kampeni ya awamu ya nne ulikwama kuendeleza harakati zake katika kuiandaa awamu ya tano.

Hivi karibuni kuhamia upinzani ACT-Wazalendo kwa Bernard Membe, kulifanana kwa njia fulani na kuhama mwaka 1995 kwa Augustine Mrema, aliyetoka CCM na kwenda NCCR-Mageuzi, kwa kuwa alikuwa ni mtu mwenye dhamira ya kugombea urais

Wakati huo, nafasi yake kuwania urais ndani ya CCM ilikuwa ni kitendawili aliamua kuhama.

Kimsingi, kwa wakati ule ilionekana ni ‘kipindi kilichokubalika’ au ‘muafaka’ kwani upinzani ulikuwa mchanga na haukuwa na vigogo wa kutosha kuubeba kwa nafasi hiyo nzito.

Mwaka huu ni ghafla, ilishuhudiwa jambo jipya ambalo wengi hawakuliamini, Tundu Lissu kupitishwa na chama chake kuwania nafasi ya urais na hatimaye akahitimisha

dhamira yake, hata akijitosa kampeni na kushiriki uchaguzi, kabla ya kurudi tena barani Ulaya.

Je, ni sahihi kusema kambi ya upinzani uimara wake katika kusimamisha urais, ni sharti awe mwanasiasa ‘kigogo’ aliyehama kutoka ng’ambo nyingine kama historia inavyojieleza?

Kwa kurejea matokeo ya uchaguzi mkuu wa hivi karibuni majibu yake yanabaki njiapanda.

Itakumbukwa kuwa mwaka 1995 waziri mwandamizi, Augustine Mrema, baada ya sintofahamu muda mfupi kabla ya uchaguzi mkuu, kupitia kisichotegemewa wakati huo ghafla, alihamia NCCR-Mageuzi, na kuvikwa ugombea urais.

Katika uchaguzi wa mwaka 2005, CHADEMA ikipeperusha bendera yake ya urais, kwa mgombea Freeman Mbowe, matokeo hayakuwa rafiki kwa kuambulia kura ‘kiduchu’ na vyama vingine hali ilifanana.

Pia ndani ya CHADEMA, Katibu Mkuu wake, Dk.Wilibrod Slaa, aliyekuwa sehemu ya mzizi muhimu, mwaka 2010 aligombea nafasi hiyo ya urais na kutoa ushindani mkubwa.

Baada ya miaka mitano naye alinyanyua virago na kurudi CCM,

> Itakumbukwa kuwa mwaka 1995 waziri mwandamizi, Augustine Mrema, baada ya sintofahamu muda mfupi kabla ya uchaguzi mkuu, kupitia kisichotegemewa wakati huo ghafla, alihamia NCCR-Mageuzi, na kuvikwa ugombea urais.

kisa na mkasa kuruhusiwa Lowassa kugombea urais kwa tiketi ya CHADEMA, mtazamo wa hamaki ambao ulimsibu pia Mwenyekiti na mgombea urais wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba.

Ni suala walilolijadili kwa muda mrefu, kuwa Slaa na Profesa Lipumba, ni vipi kumpokea mkongwe huyo wa kisiasa CHADEMA, ili apeperushe bendera ya upinzani, pamoja na kuwa uwezekano wa kupata viti vingi zaidi vya ubunge?

Hivyo, kwa mantiki ya tathmini ya sayansi ya siasa, ujio wa Lissu safari hii na huenda hata kukwama kwake kufanikisha dhamira yake pamoja na chama katika uchaguzi uliopita si jambo jipya ndani ya miaka 28 ya Tanzania ya siasa za vyama vingi, katika awamu ya pili baada ya uhuru.

Ishara iliyoko sasa kwenye ubao wa siasa za upinzani kwa zama za sasa, hakuna tofauti kubwa na yanayoendelea kujiri tangu uchaguzi mkuu wa 2005.

Alipoibuka katika nafasi nyingine ya uteuzi wa kidiplomasia, Dk. Slaa, Katibu Mkuu wa zamani wa CHADEMA, akawa anasikika kuwa anang’ara kwa uwajibikaji akiwa Balozi nchini Sweden.

Muonekano wa Dk. Slaa ni wa aina yake, hivi sasa akiwa ni

> Alipoibuka katika nafasi nyingine ya uteuzi wa kidiplomasia, Dk. Slaa, Katibu Mkuu wa zamani wa CHADEMA, akawa anasikika kuwa anang’ara kwa uwajibikaji akiwa Balozi nchini Sweden.

kamisaa wa kisiasa, mwenye nyayo ndani ya siasa halisi za chama tawala na ngome kuu ya upinzani.

Ni mazingira yanayoshuhudiwa, Dk Slaa si wa kwanza kwa mfumo wa mwenendo, mtu anatoka CCM na kuhamia upinzani, ama anapata mafanikio au lah , anapokutana na magumu anarejea tena kwenye kimbilio nyumbani.

Ni kwa mrejeo huo huo wa tathmini ya sayansi ya siasa, CCM inasimama katika nafasi ya nguzo ya kitaifa.

Simulizi hizo zinaweza kwenda mbali, kwa historia ya safari za waliokuwa mawaziri wakuu kwa ‘kuachiana ziwa’ Lowassa na Frederick Sumaye, wote walitua CHADEMA kila mmoja kwa safari yake.

Leo hii, historia inajirudia kwa kanuni ile ile ya msingi, kila mmoja kwa wakati wake amesharejea kundini CCM, wakitambuliwa na ‘mzazi’ kwa kukaribishwa katika dhifa za kitaifa na hafla nyinginezo kwa heshima ya nafasi zao serikalini.

Tathmini ya jumla, inaibeba CCM kisiasa na katika nafasi yake ya chama tawala kwamba imebeba taswira tofauti ya wakongwe wake, wageni na waliorejea nyumbani ikiipatia sura ya kitaifa.



Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk. Willboard Slaa.



Mgombea urais wa CHADEMA 2020, Tundu Lissu.



Bernard Membe, aliyegombea urais kwa tiketi ya ACT –Wazelendo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MGOGORO ETHIOPIA

# Tofauti za kipato, kubeba ukabila, kunavyoitumbukiza Ethiopia vitani



Abbas Mwalimu

**Na Sabato Kasika**

ETHIOPIA imekumbwa na vita vinavyohusisha vikosi vya jeshi la serikali ya jimbo la Tigray na majeshi ya serikali ya shirikisho.

Abbas Mwalimu mchambuzi wa siasa, anazungumza na Nipashe na kueleza kuwa kiini cha vita hivyo ni mlolongo unaoanzia kwenye ukabila, umaskini na tawala za majimbo.

Mchambuzi huyo anasema, serikali ya jimbo la Tigray iliyokuwa ikiongozwa na Rais wa jimbo hilo Debretsion Gebremichael , wa chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), ni sehemu ya chama kikuu cha Ethiopia People's Revolution Revolutionary Democratic Front (EPRDF).

"Ni muungano wa vyama vinne vya kikabila na vyama vya eneo la kusini ambalo lilikataa kutii agizo la kuahirisha uchaguzi hadi mwaka 2021 kama lilivyotolewa na serikali ya shirikisho ya Ethiopia," anasema Abbas.

Anasema, sababu kubwa ya kuahirisha uchaguzi huo iliyoelezwa na Waziri Mkuu Dk. Abiy Ahmed, ni kuwapo ugonjwa wa COVID-19 unaosumbua nchini humo.

"Hadi sasa mgogoro huo umesababisha watu zaidi ya 27,000 kukimbilia nchi ya Sudan huku watoto zaidi 2,000,000 wakihitaji msaada wa dharura," anasema akinukuu taarifa za Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) na la Haki za Binadamu la Amnesty International.

Anasema, licha ya Waziri Mkuu Ahmed kusuluhisha mgogoro baina ya Ethiopia na Eritrea ulioanza mwaka 1998, nchi hiyo imeendelea kukumbwa na tishio la mapinduzi mara kwa mara.

**KIINI CHA MGOGORO**

Mwalimu anasema kiini kimejikita kwenye tofauti kubwa kati ya walio nacho na mafukara kwa misingi ya ukabila.

"Ethiopia imekuwa na tatizo la tofauti kubwa ya kipato kati ya matajiri na maskini miongoni mwa makabila makuu ya Waoromo, Waamhara, Wasomali, Watigri, Wasidama, Wagurage, Waloyta, Waafar na wengine tangu miaka ya 1960, hasa linapokuja swali na nani anapata nini katika keki ya taifa," anasema Mwalimu.

Anasema, suala la kukosekana usawa kwa misingi ya kufungamana na ukabila, limekuwa sehemu ya utawala wa serikali ya Ethiopia tangu kuzaliwa kwa madola yaliyopo sasa na mwishoni mwa karne ya 19.

"Kuanzia mwaka 1648, Amhara lilichukuliwa kama kabila pekee linaloongoza taifa na mtu yeyote aliyetaka kupata nguvu za kisiasa ama ajira katika uongozi wa nchi ilimpasa kuwa mfuasi wa dini ya Urthodox, anayefahamu Kiamhara," anasema.

Mchambuzi huyo anasema mgogoro unahusisha matajiri dhidi ya wafanyakazi na kwamba wanyonyaji hao wanamiliki njia za uzalishaji mali na hutaka kuwatumikisha wafanyakazi, jambo linalozua migogoro.

" Chama EPRDF kilikuja na mikakati miwili ya kutatua tofauti za kipato kati ya walio nacho na wasio na kitu iliyojengeka katika misingi ya ukabila," anasema.

"Ukitazama kwa Ethiopia kutokana na mgawanyiko wa serikali za majimbo za kikabila, ni wazi suala la kuahirishwa kwa uchaguzi mpaka 2021 kutokana na COVID-19 ilikuwa ni sababu ya kutaka kujitenga kwa jimbo la Tigray na si kingine, kwani hata Amhara walijaribu kufanya mapinduzi mwaka 2019 huku Sidama wakipiga kura ya kujitenga," anasema.

**UTATUZI WA MGOGORO**

Mwalimu anataja mkakati wa kwanza kuwa ni kuondoa matabaka kati ya maskini na matajiri kwa kuyatazama makabila kama chombo cha kujenga shirikisho la Ethiopia.

"Mkakati wa pili ni kuzitumia kanuni za Joseph Stalin (Stalin Principles) zinazounda serikali za majimbo kwa kutoa haki ya kila sehemu kujitawala.

"Abiy alizutumia kanuni hizi kuweka mfumo wa serikali za majimbo ya kikabila kujitawala na hata kujitoa katika serikali ya shirikisho pale zinapoona vigezo fulani vimetimia," anasema.

Mwalimu anaeleza kuwa tangu kuingia madarakani chama cha EPRDF 1991 kulifanyika majaribio kadhaa ya kutatua mgogoro wa kikabila unaoitafuna Ethiopia ikiwamo kuweka mikutano ya kitaifa.

Anafafanua kuwa lengo la mikutano hiyo likiwa ni kuunda katiba mpya, ambayo ilitambua serikali za majimbo yanayojitawala, yakiwa na marais na serikali zao na kusaidia kupunguza migogoro ya wenyewe kwa wenyewe.

"Kwa mantiki hiyo, Ethiopia ilianza kuwa na mfumo wa serikali za majimbo yanayojitawala kikatiba na ndiyo mfumo unaoendelea hadi sasa huku majimbo hayo yakiwa na uwezo wa kujitenga na kuwa nchi huru," anasema Mwalimu.

Anasema, hilo linawezekana ikiwa yatahitaji kufanya hivyo, kwa kupiga kura ya maoni, na kwamba jimbo la Sidama lilifanya hivyo Novemba mwaka jana.

**MAKOSA YALIPOANZIA**

Mwalimu anasema, swali la msingi liliibuka baada ya EPRDF kuunda serikali ya shirikisho ya majimbo ya kikabila yanayojitawala na kuhoji mpango huo ungeleta umoja wa kitaifa?

"Kwa bahati mbaya zaidi tofauti na kilivyotegemea chama cha EPRDF, serikali ya shirikisho ya majimbo yanayojitawala ilisababisha kupotea kwa umoja wa kitaifa na kuongeza mgawanyiko na matabaka," anasema Mwalimu.

Mgawanyiko huo wa matabaka ulivutia baadhi ya makabila kutaka kujitenga kutokana na kuimarika kwa tawala za kikabila na kwamba wachambuzi wa siasa za Ethiopia wanabainisha hilo.

"Serikali ya shirikisho ya majimbo ya kikabila imesababisha nchi kugawanyika na kuingia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe kutokana na kuwa na serikali zake, mabunge yake na mahakama zake," anasema Mwalimu.

Wanasayansi wa sayansi ya siasa wanaamini kwamba muundo wa taasisi hutoa nafasi ya kukusanya mahitaji ya makabila na jamii zote katika nchi husika ili kuondoa uwezekano wa migogoro.

Inaonekana Ethiopia ilivuruga kwenye katiba kuruhusu majimbo ya kikabila kujitawala, anasema.

Anasema, kupitia katiba, mfumo wa siasa kiuongozi unaweza kujengwa kwa kuweka uwiano baina ya makundi ya walio wachache na walio wengi, kuhakikisha wote wanawakilishwa katika uongozi wa taifa na kutoa nafasi kwa ushiriki wa wote.

**MIGOGORO KUTOKWISHA?**

Mwalimu anasema, serikali za majimbo zinajiona kuwa na uwezo wa kujitawala na kujipangia mambo yao wenyewe, huku serikali ya shirikisho ikihakikisha inasimamia mustakabali wa majimbo hayo kuzingatia sera za kiuchumi na kiusalama jambo linaloleta mtafaruku.

Anasema, kutokana na mazingira hayo kila serikali hutunisha misuli kuwa ndiyo ina haki ya kusimamia ustawi wa eneo lake , ndipo mitafaruku inapoanzia.

Wale wenye uchu wa madaraka huichokonoa serikali ya shirikisho ili vita itokee ili kujitwalia mamlaka na madaraka ya kuongoza maeneo hayo kama nchi kamili.

"Ukitazama kwa Ethiopia kutokana na mgawanyiko wa serikali za majimbo za kikabila, ni wazi suala la kuahirishwa kwa uchaguzi mpaka 2021 kutokana na COVID-19 ilikuwa ni sababu ya kutaka kujitenga kwa jimbo la Tigray na si kingine, kwani hata Amhara walijaribu kufanya mapinduzi mwaka 2019 huku Sidama wakipiga kura ya kujitenga," anasema.

Anasema, uwepo wa serikali za majimbo za kikabila umeongeza ari ya watu wa makabila kujitazama kwa misingi ya kikabila na kuongeza kujitambua kwa kabila moja dhidi ya jingine, hivyo kupunguza hali ya utaifa na hatimaye kupoteza umoja uliokusudiwa.

"Bado kuna uwezekano wa kutatua mgogoro huu, hasa Umoja wa Afrika (AU) kutumia marais na mabalozi wanaoelewa mila na desturi na utamaduni wa makabila ya Ethiopia kufikia suluhisho," anasema.

Mwalimu anasema AU inaweza kusuluhisha mgogoro huo, ikiwamo kupeleka vikosi vya ulinzi wa amani. Yote yatategemea utayari wa Serikali ya Shirikisho ya Ethiopia na AU.

JUKWAA LA UONGOZI

# KIJANA BOBI WINE

## ■Waridi, chipukizi wa mapinduzi la Afrika
## ■Ataondoa utamaduni wa 'vibabu' kufia ikulu?



Robert Kyagulanyi au Bobi Wine, mgombea urais wa Uganda mwenye mvuto kwa vijana. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

AFRIKA inatajwa kuwa ni bara changa linaloongozwa na wazee ni kwa sababu marais wengi wenye zaidi ya miaka 70 wako ikulu bila kuwapa nafasi vijana ambao ni takribani asilimia 60 ya raia wote.

Umoja wa Afrika(AU) umeanzisha kampeni ya 'The Africa We Want' au Agenda 2063' ambayo inasimamia mtangamano wa kweli wa Afrika ifikapo mwaka 2063 ambao bila shaka, viongozi wa miaka 70 haliwezi kuwa jukumu lao.

Bobi Wine anakuwa kijana wa kwanza Afrika kutaka kuwatoa ikulu mababu. Anataka kubadilisha sura ya kisiasa kwani kuanzia sasa hapana shaka yumo kwenye uchaguzi mkuu wa Uganda mwaka huu, akimpinga Rais Yoweri Museveni.

Bobi Wine au Robert Kyagulanyi Ssentamu,yupo na hii ni baada ya Tume ya Uchaguzi ya Uganda kumteua mwanamuziki huyo maarufu aliyegeuka mwanasiasa wa upinzani, kuwa mgombea rasmi wa urais katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani

Kyagulanyi ameibuka kuwa hasimu mkuu wa kisiasa wa rais wa muda mrefu wa taifa hilo Yoweri Museveni, lakini uteuzi wake ulielezwa kuwa ulikumbana na mkono wa chuma wa jeshi polisi, ambalo lilimkamata na wafuasi wake kupambana na vikosi vya usalama wakati wakishangilia uteuzi wake.

Huyo ndiye mwanasiasa na msanii Robert Kyagulanyi almaarufu Bobi Wine akiwaongoza wafuasi wake wachache waliomsindikiza kuteuliwa na tume huru ya uchaguzi.

Akizungumza mara baada ya uteuzi wake, Bobi Wine, anasema anawania nafasi hiyo ya juu ya kuwaongoza Waganda ili kuwawakilisha watu wanaokandamizwa, walio dhaifu, maskini na wenye kudhulumiwa miongoni mwa wengine .

"Natumia wakati huu kutangaza kwamba tunachoshuhudia sasa ni uzinduzi wa awamu muhimu katika mapambano yetu ya kuikomboa nchi yetu kutoka kwenye minyororo ya udikteta uliotukwamisha kwa karibu miongo minne. Tumevifunga vitabu vya malalamiko. Sasa tumefungua kitabu cha vitendo. Niko hapa kumnusuru rais Museveni kutokana na yeye mwenyewe; kutokana na rushwa yake na ulezi wake miongoni mwa mengine.

> "Natumia wakati huu kutangaza kwamba tunachoshuhudia sasa ni uzinduzi wa awamu muhimu katika mapambano yetu ya kuikomboa nchi yetu kutoka kwenye minyororo ya udikteta uliotukwamisha kwa karibu miongo minne. Tumevifunga vitabu vya malalamiko. Sasa tumefungua kitabu cha vitendo. Niko hapa kumnusuru rais Museveni kutokana na yeye mwenyewe...

### KUTISHIA WAKONGWE

Mgombea huyo wa urais anakiwakilisha chama cha upinzani cha National Unity Platform (NUP), ni kijana mdogo anayeonekana dhahiri kuwa anakitishia kizazi kikongwe cha viongozi wa Afrika.

Afrika bara changa linaloongozwa na wazee, ni wazi haliko tayari kumpokea mtoto huyu, kubadilisha mwelekeo.

Kyagulanyi kama ambavyo hakuna anayeweza kumpa nafasi ya kumpokonya unga mzee mzima, anakutana na kibano cha polisi na kulazimika kusimamisha kampeni zake wiki iliyopita.

Bobi Wine alitangaza kurejea kwenye kampeni wiki hii baada ya kukamatwa katika eneo la Luuka na kupelekwa kituo cha polisi cha Nalufenya.

### KUANDAMWA KUPINDUKIA

Uchaguzi wa Uganda una wagombea 11 wanaowania kiti cha urais katika uchaguzi mkuu wa Uganda, akiwamo kigogo Yoweri Museveni na majenerali wake wawili wa zamani wanaoelezwa kuwa walikuwa naye vitani kabla ya msituni kabla ya kuingia madarakani.

Hata hivyo anayeandamwa na dola ni Bob Wine ambaye katika kushangilia uteuzi wae watu karibu 50 walikamatwa kufuatia shamra shamra za kushangilia uteuzi zilizotokea katika mji mkuu wa Kampala baada ya mwanasiasa huyo kuidhinishwa kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwezi Januari mwaka 2021.

Mgombea huyo hakupewa nafasi ya kufurahia uteuzi badala yake alisukumizwa kwenye karandinga la polisi muda mfupi baada ya uteuzi wake wa urais na haikuwezekana kushangilia pamoja na wafuasi wake kwani alikimbizwa nyumbani na kuziliwa.

Anakwamishwa kila mahali na hata siku alipotaka kwenda kuzindua ilani yake ilikuwa vigumu pia.

Mgombea huyo anayeteka hisia za vijana na mwenye uwezekano wa kupiiwa kura nyingi na kundi hilo ni mwanzo wa kizazi kipya kutaka kuiteka ajenda ya 'the Africa We Want'.

### AFRIKA YA VIKONGWE

Viongozi wa Afrika wengi hawako tayari kung'atuko miongoni mwao ni mkongwe Robert Mugabe, wa Zimbabwe, aliyefariki Septemba mwaka jana ,alifurumushwa ikulu 2017, baada ya kutawala kwa miaka 37.

Kigogo mwingine ni aliyeondoka madarakani mwaka 2017 ni José Eduardo dos Santos Rais wa Angola, akistaafu baada ya miaka 38 . Kiongozi huyu anatuhumiwa kuwaacha wanae wawili kwenye nafasi nyeti za uongozi serikalini.

Mkongwe Yahya Jammeh, Rais wa Gambia, naye alikabidhi madaraka kwa shinikizo la jesho lililosimamiwa na askari wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Magharibi ECOMOG, akitakiwa kukubalika matokeo na kuondoka kwa vile chama chake kilikuwa kimeshindwa. Alitumbuliwa akiwa na miaka 23 ya kuwa kiongozi wa taifa hilo aliyeingia madarakani kwa njia ya mapinduzi.

Aprili 2019 nchini Sudan iliandikwa historia rais wa zamani Omar al-Bashir, baada ya miaka 30 ya utawala wa chuma, aling'oka baada ya maandamano ya kumpinga yaliyochukua miezi kadhaa raia wakishinikiza kuwa hawamtaki pamoja na chama chake.

Mwaka huu ulianza kwa kumng'oa madarakani Abdelaziz Bouteflika, aliyelazimika kujiuzulu kama rais wa Algeria, kutokana na kushinikizwa na maandamano ya kumpinga kufuatia tangazo kuwa angegombea tena mara ya tano kwenye nafasi ya urais

Huko Equatorial Guinea, Teodoro Obiang Nguema, amekuwa rais kwa miaka 40 baada ya kuiangusha serikali iliyokuwa inaongozwa na mjomba wake Francisco Macías Nguema ambaye baadaye aliuawa.

Kadhalika nchini Rwanda, Paul Kagame, haonyeshi dalili za kuondoka ikulu tangu alipoingia madarakani miaka 25 iliyopita. Pamoja naye Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, anayegombea awamu nyingine kwenye uchaguzi mkuu.

***MITANDAO.***



## Kongamano kuwakutanisha wadau sekta afya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JUMLA ya wadau 354 kutoka nyanja mbalimbali ya sekta ya afya wanatarajia kushiriki kongamano la afya litakalofanyika kuanzia leo na kesho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Rais wa kongamano hilo, Dk. Omary Chillo, alisema kongamano hilo ni la saba kufanyika na lengo ni kujadili uchumi wa kati unavyoendana na nyanja ya afya nchini.

Dk. Chillo alisema katika kongamano hilo, tasisi zisizo za kiserikali zitatoa mada na kujadili ni jinsi gani hasa wataweza kuboresha afya ya jamii kwa wananchi.

Alieleza kuwa katika mkutano huo watatoa mrejesho wa mikutano mingine iliyowahi kufanyika na kutoa mapendekezo ya nini hasa kifanyike katika kuboresha sekta ya afya kipindi hiki cha uchumi wa kati.

"Msingi mkuu wa kongamano hili ni kubadilisha uzoefu na kuona tunafanyaje kazi hasa kipindi hiki tulichoingia uchumi wa kati katika taifa letu pendwa la Tanzania," alisema.

Vilevile, Dk. Chillo alisema kutakuwapo na maonyesho mbalimbali ya masuala ya afya na wabunifu watakaoshiriki katika kongamano hilo watapatiwa zawadi.

"Natoa wito kwa watu ambao bado hawajajiandikisha kujiandikisha ili kushiriki kongamano hilo, na kuleta chachu katika sekta ya afya na kuboresha mifumo ya afya zaidi nchini," alisisitiza.

**Natoa wito kwa watu ambao bado hawajajiandikisha kujiandikisha ili kushiriki kongamano hilo, na kuleta chachu katika sekta ya afya na kuboresha mifumo ya afya zaidi nchini.**

# Uwezo wa serikali kugundua wagonjwa wenye TB wapaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeongeza uwezo wa kugundua wagonjwa wapya wa Kifua Kikuu (TB) na kuwaweka kwenye matibabu kutoka wagonjwa 62,908 mwaka 2015 na kufikia 82,166.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma jijini hapa.

Alisema serikali imejipanga kutokomeza ugonjwa huo kwa kuongeza uwezo wa ugunduzi wa wagonjwa wapya.

Prof. Makubi alisema maisha ya wananchi takribani 300,000 wakiwamo watoto 45,000 yameponywa kwa kupatiwa dawa kwa wakati na kufuatiliwa kwa usahihi kuanzia mwaka 2015 hadi sasa.

"Juhudi hizi pia zimepunguza idadi ya vifo vinavyosababishwa na kifua kikuu kwa asilimia 33, ambapo mwaka 2015 kulikuwa na vifo 30,000 hivi sasa vimepungua hadi kufikia vifo 20,000," alisema.

**Malengo ambayo tulijiwekea ya kupunguza vifo vitokanavyo na kifua kikuu tumeweza kuyafikia pamoja na kupunguza madhara yanayotokana na ugonjwa huo.**

Prof. Makubi alisema mafanikio hayo ya ongezeko la kasi ya ugunduzi wa wagonjwa wapya yametokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma.

Alieleza kuwa mikakati hiyo ni kuboresha huduma za ugunduzi wa TB na kutoa kipaumbele kwa makundi yaliyoathirika zaidi kama kaya zenye wagonjwa, wanaoishi kwenye kaya duni, gerezani, wachimbaji wadogo na kwa waathirika wa dawa za kulevya.

"Aidha, tumewekeza katika afua bunifu mbalimbali za matumizi ya teknolojia mpya za molekyula za kubaini TB kwa usahihi na kwa haraka," alisema Prof. Makubi.

Awali Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Leonard Subi, alisema wizara imefanya vizuri kwenye kwa kufikia malengo waliyoyaweka kwenye mpango mkakati ambao unamalizika mwaka huu.

"Malengo ambayo tulijiwekea ya kupunguza vifo vitokanavyo na kifua kikuu tumeweza kuyafikia pamoja na kupunguza madhara yanayotokana na ugonjwa huo," alisema.

Pia, alisema kuwa serikali imefanikiwa kuongeza vituo vya upimaji wa kifua kikuu sugu kutoka kituo kimoja mwaka 2015 hadi kufika vituo 145.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo imejiwekea mikakati ya kuwawezesha watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya, ili wawe na ujuzi na uwezo wa kutambua na kutoa huduma kwa wagonjwa wa TB.



Mwezeshaji wa Mradi wa Elimu Jumuishi, Fontonatus Raphael, akitoa elimu ya mafunzo kwa wadhibiti ubora wa elimu kutoka jijini Dodoma na Bahi kuhusiana ushawishi na utetezi juu ya watu wenye ulemavu yaliyofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Chanzo cha uuzaji holela pombe chawekwa wazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kutokuwapo kwa sera ya pombe, kumesababisha bidhaa hiyo kuuzwa ovyo kwenye maduka ya vyakula badala ya maeneo yenye leseni ya kufanya biashara hiyo.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, aliyaeleza hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na Mtandao wa Mashirika ya Kupambana na madhara ya matumizi mabaya ya pombe nchini (TAAnet).

Alisema kutokana na hali hiyo, unywaji wa pombe kupita kiasi umekuwa ukisababisha athari kwa jamii ikiwamo vitendo vya ukatili wa kijinsia, kupoteza nguvu kazi ya vijana na kudumaza maendeleo ya kiuchumi.

Mbunge huyo alisema kuna sheria ya pombe na vilevi ya mwaka 1968 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 1977, lakini zimepitwa na wakati na bado hakuna sera ya utekelezaji wa sheria hizo.

Alibainisha kuwa sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho tena mwaka 2009 imezingatia zaidi matangazo ya kibiashara na matumizi bila mipaka.

"Mimi kama mbunge nitahakikisha tunaanza kufanyia kazi kwa kuwa ndio Bunge kwanza litaanza kazi zake Februari 2, mwakani, itabidi tufanye utaratibu wa kuwafikia wabunge wapya ili kuwa na sauti ya pamoja ili kufanikisha kuwepo na sera," alisema.

Aidha, alisema ni muhimu kuwapo kwa sera ambayo haitaathiri viwanda na wawekezaji, lakini ambayo itasimamia sheria miongozo sahihi ya matumizi ya pombe.

"Maana kuna watu wanatuma hata watoto wadogo kuwanunulia bia na akipewa anaonja, hii si nzuri inahitaji kuokoa kizazi kijacho," alisema.

Aliwaasa waandishi kuandaa vipindi na makala mbalimbali zinazotoa elimu ili jamii ifahamu madhara ya matumizi ya pombe kupita kiasi.

Awali, Mwenyekiti wa Mtandao huo, Sophia Komba, alisema mafunzo hayo kwa waandishi yanalenga kusaidia kuandika habari zinazochochea uwepo wa sera ya kudhibiti unywaji pombe kupita kiasi.

Alisema kuwa sheria zilizopo zinapuuzwa kwa kiasi kikubwa na watu wanafanya biashara ya pombe bila kufuata sheria.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo bado hazina sera ya pombe au mwongozo kuhusu matumizi ya pombe ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya, Malawi na Zambia wakati wenzetu wa Uganda, Burundi na Rwanda wamepiga hatua katika upatikanaji wa sera," alisema.

Alisema lazima kuwapo kwa mifumo mizuri ya uuzaji wa pombe kwa kuzingatia umri wa muuzaji, mnunuzi, siku, muda na mahali pakuuzia.

Akizungumzia hali ya unywaji wa pombe kimataifa, mwenyekiti huyo alisema takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2018 zinaonyesha matumizi mabaya ya pombe yamesababisha vifo vya watu milioni tatu ikiwa ni asilimia 5.3 ya vifo vyote.

Alisema watu wanaofariki kwa sababu hiyo idadi yao ni kubwa kuliko wanaofariki kwa ugonjwa wa kifua kikuu, Ukimwi, na sukari, huku wanaume ndio wanaoongoza kwa vifo.



# Chanzo maradhi ya meno chatajwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MFUMO mbovu wa ulaji na kutofanya usafi wa kinywa kwa baadhi ya Watanzania umetajwa kuwa chanzo cha watu wengi kuugua maradhi ya kinywa na meno ikiwamo kansa ya kinywa.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mbeya na Katibu wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA), Dk. Ngemma Berege, wakati wa maadhimisho ya miaka 40 tangu chama hicho kilipoanzishwa, yaliyofanyika mjini hapa.

Maadhimisho hayo yalifanyika kwa jopo la madaktari hao bingwa wa kinywa na meno kushirikiana na madaktari bingwa wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kutoa huduma ya matibabu bure kwa wananchi wanaosumbuliwa na maradhi ya kinywa na meno.

Dk. Berege alisema wananchi wengi wamekuwa wakitumia mara kwa mara vyakula vyenye sukari nyingi bila kusafisha meno hali ambayo ndiyo chanzo kikubwa cha maradhi hayo.

**Meno na kinywa vinahitaji kutunzwa vizuri. Tatizo kubwa linalowakabili Watanzania wengi ni kutokula mlo kamili ambao unajumuisha vyakula vya kuimarisha meno.**

"Mfumo wa ulaji unaathiri sana kinywa na meno. Kuna mtu kila akihisi kiu anatamani kunywa kinywaji fulani, sasa anakunywa hivyo vinywaji vyenye sukari na hakumbuki kusafisha meno kama inavyotakiwa, hivyo kujiweka katika hatari ya kupata maradhi haya," alisema Dk. Berege.

Ili kudhibiti madhara zaidi ya kinywa na meno, aliwataka Watanzania kubadili mfumo wa ulaji kwa kuepuka kula mara kwa mara vyakula vyenye sukari nyingi pamoja na kukumbuka kusafisha kinywa mara kwa mara.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam Ndaki ya Mbeya, Dk. Emeria Mugonzibwa, aliwataka Watanzania kula vyakula vyenye madini yanayosaidia kuimarisha meno yakiwamo madini ya kalshiamu.

Pia alishauri watu kuzingatia utunzaji wa kinywa kwa kusafisha meno kwa kutumia dawa zenye madini yanayoimarisha meno na kuua wadudu wanaoshambulia kinywa na meno.

"Meno na kinywa vinahitaji kutunzwa vizuri. Tatizo kubwa linalowakabili Watanzania wengi ni kutokula mlo kamili ambao unajumuisha vyakula vya kuimarisha meno," alisema Dk. Mugonzibwa.

Katika maadhimisho hayo, watu 19 wenye matatizo ya kinywa na meno kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walinufaika na huduma ya upasuaji wa kinywa na meno iliyotolewa bure na madaktari hao.

Daktari bingwa wa kinywa na meno wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Lazaro Mboma, aliwaomba madaktari bingwa kufika mara kwa mara hospitalini hapo kusaidia utoaji wa matibabu kwa wananchi ambao wengi hawana uwezo kiuchumi.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Akson (kulia), akizungumza na waandishi wa habari juzi, kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo kuanza utekelezaji wa ahadi alizoahidi wakati wa kampeni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watakiwa kugeukia mambo ya maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kusahau habari za uchaguzi mkuu ambao umeshapita na badala yake waendelee kukitumikia chama kwa uadilifu ili kufikia ndoto zao za kisiasa.

Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alitoa ushauri huo juzi jijini hapa alipokuwa anakabidhi vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kukamilisha nyumba ya makazi ya Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) wa Mkoa wa Mbeya ambayo inajengwa katika Kata ya Itezi.

Mwaselela ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Uchumi na Fedha ya CCM Mkoa wa Mbeya, alisema yeye ni miongoni mwa watu waliosomeshwa na chama hicho, hivyo anatamani vijana wafanye kazi kwa uaminifu.

Alisema wanachama wote wa chama hicho wanatakiwa kuachana na masuala ya uchaguzi na sasa waendelee kuchapa kazi ili kujiinua kiuchumi.

Katibu wa UVCCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Steven Shija, alisema baada ya uchaguzi mkuu kukamilika, vijana wameanza kuhimizana kufanya kazi kwa bidii ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema wakati wa uchaguzi kulikuwa na mgawanyiko mkubwa wa wanachama wa chama hicho na kwamba baadhi walikuwa wanaitana majina ya ajabu ajabu, lakini baada ya uchaguzi kuisha na makundi kuvunjwa, wanachama wameanza kuwa wamoja.

Baadhi ya vijana waliohudhuria makabidhiano hayo, waliahidi kufuata nyayo za mdau huyo wa maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii ili na wao wajikwamue kiuchumi.

# DC ataka mafunzo usalama, afya kwa wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imesema kuna haja ya kuwawezesha watu wenye ulemavu katika shughuli za uzalishaji kupitia mafunzo ya usalama na afya kazini na kuwapa mitaji ili kuboresha shughuli zao za kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kukuza uelewa wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yalioandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) Mkoa wa Mbeya.

Ntinika ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo, alisema: "Serikali imetenga fungu maalum la fedha kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba kwa makundi mbalimbali katika jamii ambapo asilimia 2 ya fedha hizo ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Aliongeza kuwa: "Kama serikali tunaona kuna umuhimu wa kutoa mafunzo ya usalama na afya kwa makundi lengwa, ili waweze kuepuka madhara yanaweza kusababishwa na kutozingatia kanuni za usalama na afya kazini," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alipongeza OSHA kwa kutekeleza ipasavyo wajibu wake ikiwamo kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu nyingi za kazi pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya afya na usalama kazini.

Hata hivyo, Ntinika aliitaka OSHA kuongeza jitihada zaidi ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mafunzo hayo ya siku moja yalijikita katika kuainisha na kushauri mbinu za kudhibiti vihatarishi vya usalama na afya ambavyo huambatana na shughuli mbalimbali za uzalishaji zikiwamo ujenzi, kilimo, ufundi seremala, kilimo, ufugaji, biashara ndogo na kazi za ofisini.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo watu wenye ulemavu katika mikoa mbalimbali na kusisitiza kwamba ni endelevu.

"Kama taasisi yenye dhamana ya usalama na afya kwa mfanyakazi, tumeona kuna umuhimu wa kuyafikia makundi haya ya watu wenye ulemavu kwa kuwa tunatambua ulemavu ni hali tu na haupaswi kuwa kikwazo kwa mtu kushiriki katika shughuli kiuzalishaji." Alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Renatha Xavery, ambaye ni mwanafunzi wa ufundi katika Chuo cha VETA Mbeya, alieleza kufurahishwa na mafunzo hayo na yatawawezesha kujilinda dhidi ya vihatarishi mbalimbali vilivyopo katika sehemu zao za kazi.

"Mafunzo haya tuliyoyapata leo tumeyaona yana faida nyingi kwani yatatusaidia kulinda afya zetu na kupitia mafunzo haya tutakuwa waangalifu zaidi katika kazi mbalimbali ambazo ni hatarishi hususan kuzingatia matumizi sahihi ya vifaa kinga muhimu," alisema.





# Makamu wa Pili ahofia ubovu mashine uwanja wa ndege

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, amesema ubovu wa baadhi ya mashine za kukagulia abiria na mizigo kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, unaweza kutoa mwanya kwa wafanyabiashara kuendesha biashara haramu na kuliingiza taifa mahali pabaya.

Aliyasema hayo juzi wakati alipofanya ziara katika viwanja hivyo, Kisauni nje kidogo ya mji wa Zanzibar kuwa ubovu wa mashine katika eneo hilo haukubaliki kwa sababu ni eneo muhimu kwa uchumi wa taifa.

Alisema hajaridhishwa na uwezo wa baadhi ya mashine zisizofanya kazi wakati serikali imeshajipanga kuona uwanja huo unatoa huduma za kimataifa.

**hajaridhishwa na uwezo wa baadhi ya mashine zisizofanya kazi wakati serikali imeshajipanga kuona uwanja huo unatoa huduma za kimataifa.**

Alisema viwanja vya ndege na bandari ni sura ya nchi ambayo lazima wageni wanapoingia wapokewe kwa kiwango kinachokubalika hatua inayokwenda sambamba na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya taifa.

Alisema kuwa viongozi na watendaji wanapaswa kuandaa mbinu na mfumo utakaosaidia serikali iongeze vianzio vyake vya mapato vitakavyoonekana na kuridhiwa moja kwa moja na wananchi.

Kadhalika alisema uwanja wa ndege unahitaji mabadiliko makubwa ili changamoto zilizopo zipatiwe ufumbuzi badala ya tabia ya baadhi ya viongozi na watendaji kusubiri ziara za viongozi katika maeneo yao.

"Uwanja wa ndege unahitaji mabadiliko makubwa, mambo yanayowezekana yasisubiri kuongozwa, na ile tabia ya watendaji kuendelea kuangalia mitandao ya kijamii ofisini kwa sasa lazima iishe," alisema Hemed.

Akizungumzia suala la mikataba, aliwaagiza wanasheria wa taasisi za umma kuangalia upya mikataba iliyotiwa saini katika miradi iliyoanzishwa kwenye taasisi zao, ili kujihakikishia mapato yanayokusanywa katika miradi ya huduma yanasimamiwa na kukidhi mahitaji halisi.

Alisema ipo baadhi ya mikataba ndani ya taasisi za umma inaonyesha dalili ya uwapo wa mwanya wa rushwa kutokana na kupungua kwa asilimia ya makusanyo ya mapato ya serikali ilhali viongozi wanaosimamia mikataba wanaendelea kushuhudia hali hiyo.

Aliutaka uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha haki za kila mfanyakazi zinapatikana ili kuondoa au kupunguza matatizo yanayowakumba baadhi yao.

Alisema wapo baadhi ya watendaji waliofukuzwa kazi kwa tuhuma mbalimbali na baada ya uchunguzi wa kina wameonekana hawana hatia, lakini bado wanaendelea kuzungushwa kitendo ambacho hakitoi haki na serikali haitaridhia kuona kinaendelea.

Kwa upande wao wahandisi wanaosimamia mashine za ukaguzi kwenye uwanja huo, walisema baadhi ya mashine hizo bado zipo kwenye uangalizi wa kampuni ilizozifungua.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Said Iddi Ndombogani, alisema wafanyakazi wanaosimamia mashine hizo hupatiwa leseni baada ya kumaliza mafunzo ya kuzihudumia.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema kitengo hicho bado kimekuwa kikikabiliwa na bajeti ndogo inayoshindwa kukidhi mahitaji halisi ya uendeshaji.

## Mawaziri waanza utekelezaji maagizo ya Rais

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAWAZIRI walioteuliwa hivi karibuni, wameanza kutekeleza maagizo 13 waliyopewa na Rais wa Zanzibar likiwamo la kukutana na wadau katika wizara zao.

Akitembelea kituo cha ufugaji wa vifaranga vya samaki juzi, Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdallah Hussein Kombo, alisema hajaridhishwa na utendaji wa kituo hicho katika kazi za kuzalisha vifaranga vya samaki, majongoo na kaa.

Alisema wizara itaunda tume ya kuchunguza mradi huo ambao kwa zaidi ya miezi 11 umesitisha shughuli za uzalishaji wa vifaranga hivyo ambavyo wateja wake ni wafugaji.

"Nimesikitishwa na uendeshaji wa kituo hiki, katika kufikia malengo yake ya udhalilishaji wa vifaranga nakusudia kuunda tume kuchunguza mradi huu," alisema Kombo.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Mussa Aboud Jumbe, alisema kituo hicho kimeshindwa kutekeleza malengo yake kwa sababu serikali haikutenga bajeti ya uendeshaji, huku Shirika la Kimataifa la Misaada ya Korea likiahidi kutoa fedha za kuendesha kituo, lakini hawakutoa.

Akizungumza na watendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Suraga, alisema uwekezaji ni kiini cha kuleta maendeleo katika nchi.

Alisema pamoja na wawekezaji kutoka nje, lakini wa ndani ni sehemu ya kuleta maendeleo hivyo ni vyema kuwsaidia ili kupata uzalishaji na kutengeneza ajira.

"Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi tunataka kutengeneza ajira 300,000 mpaka kufikia mwaka 2025, hivyo hiyo haikuwa siasa tu bali tumedhamiria na inawezekana tujikite katika kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji ili kutekeleza shughuli zao," alisema Suraga.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha inaimarisha sekta ya habari kwa kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta hiyo muhimu kwa nchini.




Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake eneo la Kwamchina Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ADA-TADEA yataka Rais Mwinyi aungwe mkono

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ADA-TADEA amewataka viongozi wa vyama vya siasa kumuunga mkono Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ili kutekeleza ahadi alizoziahidi wakati wa kampeni zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, eneo la Kwa Mchina mjini Unguja, alisema uchaguzi umekwisha na sasa ni kufanya kazi na kuachana na siasa za chuki na uhasama.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuweka maslahi ya nchi badala ya kuwa na maslahi yao binafsi kwa sababu vyama na viongozi wa vyama vya siasa watakufa, lakini Zanzibar itakuwapo.

Aliwataka wanasiasa kutii maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kutokana na Rais Dk. Mwinyi kuahidi maridhiano hayo.

"Tuweke maslahi ya Zanzibar mwanzo kuliko maslahi ya vyama vyetu...nawaomba wanasiasa namfahamu Maalim Seif ni mwanasiasa mahiri na mtu wa maridhiano hivyo kutii agizo la rais katika kutekeleza hasa kwa faida ya Wazanzibari kwa sababu maendeleo hayana chama," alisema Khatib.

Alisema chama hicho kimefurahi na mwenendo wa rais alioanza na kuwataka mawaziri walioteuliwa kutekeleza maagizo 13 waliyoagizwa na Dk. Shein baada ya hafla ya kuwaapisha mawaziri.

Alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kumteua Hemed Suleiman kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa sababu kiongozi huyo ni mchapaka kazi hodari na wakati alipokua Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba alifanikiwa kuokoa Sh. bilioni 3.5 za karafuu zilizokuwa zimefichwa kisiwani Pemba.

Pia, alisema Dk. Mwinyi ni kiongozi mbunifu ulioonekana katika kampeni zake ambazo zilikuwa za kisayansi na alikutana na makundi mbalimbali na kuzungumza nayo.

"Tunamuunga mkono uteuzi wa Baraza la Mawaziri na sisi ADA-TADEA tunamuunga mkono, kwa baraza hili amechagua chaguo sahihi wengi wao ni vijana wazalendo wenye elimu nzuri na juhudi kubwa za kufanya kazi, lakini tunampongeza rais kwa kuniteua mimi kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi," alisema.

Aliwataka wananchi kuanza kufanya utalii wa ndani ili kumuunga mkono katika kukuza sekta hiyo, kuwakaribisha na kuwafurahisha wanapokuja nchini kwa sababu ujio wao ni neema kwa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



116011802

**GERISHON PAGIEL SETH** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha nne iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **HWAZI** mwaka 2019, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **KAS/RB/5809/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EMILIANA EDWARD RAPHAEL** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NO ZA USAJILI **T439 BRE.** CHASSIS NO **AE1105035695.** ENGINE **NO 5AC066973.** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/811477/2020**

116012102

## KUPOTEA KWA PRIMARY MINING LICENCE

**EDSON EDEN MBUNDE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA **PRIMARY MINING LICENCE** YENYE NAMBA **001034NZ** ILIYOTOLEWA NA MINISTRY OF ENERGY AND MINERALS TAREHE **08/06/2017.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/816389/2020.**

116012202

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**

**DC CIVIL CASE NO.9 OF 2020**

**1) CLEMENCE MBOWE MENT..............................1ST PLAINTIFF**
**2) DIDAS PATRICE MUSHI..................................2ND PLAINTIFF**
**3) PASTORY GABRIEL TIMILA.............................3RD PLAINTIFF**

**VERSUS**

**1)JULIUS TARIMO....................1ST DEENDANT**
**2)AMAN SEMBEKE .................2ND DEENDANT**
**3)AUSTOCK ALPHONCE MUSHI...3RD DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION/HEARING**

**TO: DEFENDANT.**
Take Notice that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrates Court of Moshi on **26th the day of November 2020.** You are hereby ordered to appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any document under which you intend to rely in support of your case. **TAKE FURTHER NOTICE** that, default of your appearance on that day afore mentioned the court will proceed with the matter in your absence.

**Given under my hand and seal of this Court this 17th day of November, 2020**

**RESIDENT MAGISTRATE**
**MOSHI**

116012302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;335/2020**
**Ombi la HENRY BERNAD KOBELO, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BERNARD HENRY.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/11/2020.

Tarehe 25/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116012702

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HENRY NAFTAL SANGA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye **index namba S.5124/0011** iliyotolewa na **ST. MAXIMILIAN SEKONDARI** mwaka **2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/BUG/RB/816156/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;357/2020**
**Ombi la ANDREW JEREMIA HAULE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NEEMA NATHANIEL NSALAMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/11/2020.

Tarehe 24/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116012602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;356/2020**
**Ombi la JULITHA EMMANUEL MESSAH,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EMMANUEL MESSAH MWAKAJILA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/11/2020.

Tarehe 24/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116012502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;359/2020**
**Ombi la RAJABU RASHIDI JONGO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HASSAN TWAHIBU MSELEM.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/11/2020.

Tarehe 24/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116012602

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanahabari wamgomea Rais Yoweri Museveni

**KAMPALA, Uganda**

VYOMBO vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi Uganda, vimekataa kurusha hotuba ya Rais wa taifa hilo, Yoweri Museveni.

Hotuba hiyo ilipangwa kufanyika kila siku ya Jumapili, kuanzia majira ya saa 1:00 usiku hadi saa 3 usiku, kwa saa za Kampala.

Rais Museveni alikuwa ameagiza vyombo vyote vya habari nchini Uganda kurusha hotuba yake ya kila wiki, lakini muungano wa wamiliki wa vyombo hivyo umekataa agizo hilo, wakisema huu ni msimu wa kampeni, kwamba hawawezi kutoa fursa kwa mgombea mmoja pekee bila kuzingatia wagombea wengine kwa sababu inavunja kanuni za uandishi wa habari.

Taarifa iliyotolewa na muungano wa wamiliki wa vyombo vya habari Uganda, ikisomwa na Katibu Mkuu wake Joseph Beyanga, umeandikia Tume ya Mawasiliano Uganda - UCC, ukisema kwamba: "Rais Museveni ni mgombea wa urais katika uchaguzi mkuu mwa mwaka 2021, kwa hivyo tukipeperusha hotuba yake, wasikilizaji na watazamaji watachukulia ujumbe wake kama kampeni".

Kulingana na sheria ya utangazaji nchini Uganda ya mwaka 2013, kila mgombea katika uchaguzi anastahili kupewa nafasi sawa katika vipindi na habari zinazochapishwa au kupeperushwa na vyombo vyote vya habari nchini humo.

Kulingana na Msemaji wa Rais Museveni, Don Wanyama, hotuba ya Rais Museveni ya jumapili ilikuwa imepangiwa kuangazia usalama na ukuaji wa uchumi.

Baada ya muungano wa vyombo vya habari kukataa kurusha hotuba hiyo, Wanyama aliandika ujumbe kwenye ukurasa wa mtandao wa kijamii wa twitter kwamba: "Hotuba ya rais imeahirishwa hadi siku ambayo tutawaarifu. Tunasikitika kwa usumbufu wowote ambao umejitokeza"

Ilieleza: "Tungependa kujua aina ya hotuba atakayotoa Rais Museveni kabla ya kupanga namna ya kuirusha. Iwapo hotuba hiyo ni kampeni, basi vyombo vya habari vinavyotaka kurusha vinastahili kulipwa kwanza".

Rais Museveni mwenye umri wa miaka 76, anagombea muhula wa sita madarakani kupitia chama cha National Resistance Movement (NRM).

Machafuko yalitokea Uganda wiki iliyopita baada ya polisi kumkamata mgombea wa urais wa chama cha National unity platform - NUP, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine.

Bobi Wine alifikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka ya kufanya kampeni katika njia inayoweza kusambaza virusi vya ugonjwa wa corona. Aliachiliwa kwa dhamana na anaendelea na kampeni yake.

*DW*



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, ambaye vyombo va habari nchini humo vilimgomea kurusha hotuba yake. **PICHA: REUTERS**

# Biden ataja timu yake ya usalama, kidiplomasia

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden, ametaja timu yake ya juu ya kidiplomasia na usalama wa taifa kwa utawala wake ujao.

Kati ya walioteuliwa ni pamoja na mmoja wa washauri wake wa karibu wa masuala ya kigeni, Antony Blinken, ambaye amekuwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi.

Biden pia alimtaja mwanadiplomasia wa zamani wa Marekani, Waziri wa Mambo ya Nje, John Kerry kwa nafasi mpya kama mjumbe maalum wa rais wa hali ya hewa wakati akiwa anashikilia kiti kwenye Baraza la Usalama la Kitaifa.

Hii inaonyesha ni namna gani utawala ujao wa Biden ulivyojipanga kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa, kama suala la haraka la usalama wa kitaifa.

Biden akiwa anajiandaa kuwa rais wa 46 wa Marekani na akiwa na umri wa miaka 78, atakuwa rais mwenye umri mkubwa zaidi, wakati wa kuapishwa kwake Januari 20, huku RaisTrump akiwa anaendelea na jaribio lake la kisheria la muda mrefu la kutengua ushindi wa uchaguzi wa Novemba 3 wa kidemokrasia.

Biden, akisimamia mabadiliko yake ya kuingia madarakani Washington kutoka nyumbani kwake Wilmington, Delaware, alimchagua Alejandro Mayorkas kuwa Waziri wa Usalama wa Ndani ya Nchi.

Biden pia alimtaja Mwanadiplomasia mkongwe, Linda Thomas-Greenfield, kujiunga na Baraza lake la Mawaziri linalokuja kama chaguo lake kwa nafasi ya Balozi kwenye Umoja wa Mataifa (UN) .Nafasi hiyo inahitaji uthibitisho wa Baraza la Seneti.

Linda Thomas-Greenfield alifanya kazi katika tawala zote za wademokrat na Warepublican, wakati wa miaka 35 ya kazi katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani.

Akiwa mtaalam wa masuala ya Afrika, aliwahi kuwa Balozi wa Marekani nchini Liberia, alishikilia wadhifa hupo pia katika nchi za Kenya, Gambia na Nigeria.

Chini ya Rais Barack Obama, aliwahi kuwa Naibu Waziri anayeshughulika na maswala ya Afrika (2013-2017), akiendeleza na kusimamia sera ya Washington kuelekea bara la Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alifanya kazi pia jijini Geneva katika ujumbe wa Marekani kwenye UN.

*VOA*

# Jeshi la Ethiopia lasonga mbele Tigray

**ADDISABABA, Ethiopia**

JESHI la Ethiopia limesema liko umbali wa kilomita 60 kuufikia mji mkuu wa Tigray Mekele.

Aidha, Msemaji wa vikosi vya kundi la TPLF vinavyopambana na jeshi hilo la Ethiopia, Getachew Reda, alisema jeshi lao limeharibu kitengo cha magari ya silaha ya jeshi la serikali.

Reda, alitangaza jana kwamba wameharibu kitengo cha silaha cha Jeshi la Ethiopia, huku kiongozi wa kundi hilo la TPLF, Debretsion Gebremichael, akisema kwamba Waziri Mkuu Abiy anajaribu kufunika ukweli juu ya kushambuliwa kwa jeshi lake na vikosi vya Tigray.

Gebremichael alisema vitisho vilivyotolewa na Abiy dhidi ya Tigray ni mbinu ya kuvuta muda kutokana na kipigo walichokipata wanajeshi wake.

Kupitia Shirika la Habari la AFP, kiongozi huyo wa Tigray alisema Abiy haelewi Watigray ni kina nani.

Kadhalika, alijinadi kiongozi huyo kwamba wao ni watu wenye misimamo na wako tayari kufa kulinda haki zao kusimamia jimbo lao.

Msemaji wa serikali ya Ethiopia hakupatikana kutoa tamko kuhusiana na madai ya Tigrai. Hata hivyo Shirika la Habari la Reuters, limesema haliwezi kuthibitisha taarifa zote zilizotolewa na pande zote mbili kutokana na kukatwa kwa mawasiliano ya simu na mtandao katika eneo la Tigray.

Mamia ya watu wameuawa tangu Novemba 4, mwaka huu ulipozuka mgogoro huu na watu wapatao 40,000 wamekimbilia Sudan.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Stephanie Dujarric, akizungumza kuhusiana na hali ilivyo kwa sasa.

Kufuatia hali ilivyo Msemaji wa Katibu Mkuu wa UN, Stephane Dujaric, Alisema: ''Bado tuna wasiwasi mkubwa na usalama wa raia katika jimbo la Tigray na hasa watu zaidi ya nusu milioni ikiwamo wafanyakazi wa mashirika ya msaada 200 waliobakia Mekelle, kufuatia taarifa kwamba mapigano huenda yakaingia katika mji huo ndani ya saa kadhaa zijazo.

**DW**

**Kadhalika, alijinadi kiongozi huyo kwamba wao ni watu wenye misimamo na wako tayari kufa kulinda haki zao kusimamia jimbo lao.**

# BABA AFUNGUKA ISCO KUONDOKA MADRID



**MADRID, Hispania**

ISCO anataka kuondoka Real Madrid na kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa mujibu wa wakala wake ambaye ni baba yake mzazi, Francisco Alarcon.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake na Madrid unamalizika mwaka 2022, amekuwa na wakati mgumu wa kurudisha kiwango chake, akiwa ameanza katika mechi tatu tu za Ligi Kuu msimu huu.

Everton, Arsenal na Manchester City zimekuwa zikuhusishwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, ambaye amekuwa pale Madrid tangu mwaka 2013.

Wakala ambaye ni baba yake, Alarcon, amesema Isco anatafuta sehemu ya kwenda, ingawa pia hakutakuwa na tatizo kubaki Madrid.

"Kwa sasa, tuna ofa kadhaa, lakini Isco anataka kujaribu kwenye ligi nyingine," alisema akiiambia Cadena SER Jumatatu.

Aliongeza: "Kubaki Madrid hakutakuwa na tatizo."

Isco ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipojiunga na Madrid akitokea Malaga.



# PIRLO:

## RONALDO HAPEWI KIPAUMBELE HAPA JUVE

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo, amesisitiza Cristiano Ronaldo hapati huduma ya kipaumbele maalumu kwa miamba hao wa Serie A.

Ronaldo ameanza vizuri msimu huu akiwa na Juve, kwa kufunga mabao manane katika mechi sita.

Mabao yake mawili yaliipa Juve ushindi wa 2-0 dhidi ya Cagliari Jumamosi, na Ronaldo amecheka na nyavu mara 29 kwa Juve katika mechi 59 za Serie A mwaka huu.

Kabla ya mchezo wa jana, Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ferencvaros, Pirlo alimzungumzia Ronaldo na alisema mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, anahudumiwa kama mchezaji mwingine yeyote.

"Namchukulia Ronaldo kama wachezaji wengine, hapati huduma ya kipaumbele," alisema Pirlo akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni rahisi kuwa na mahusiano mazuri na watu wanyenyekevu. Napenda hilo.

"Namchukulia kama mchezaji mwingine yeyote kwenye kikosi changu, hivyo naona jambo zuri zaidi kwake kuonekana wa kawaida."

# MAN CITY SASA YAMTAKA GREALISH

**MANCHESTER, England**

SAHAU kuhusu Lionel Messi na Harry Kane kwani Manchester City sasa imeripotiwa kwamba inataka kumsajili Jack Grealish wakati wa dirisha la usajili la Januari mwakani.

Kwa mujibu wa gazeti la The Independent kocha wa Man City, Pep Guardiola, anataka klabu hiyo kuhakikisha inamsajili nyota huyo wa Aston Villa.

Grealish mwenye umri wa miaka 25, amekuwa nyota pale Aston Villa msimu huu na pia kuwa na wakati mzuri kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa.

Na sasa inaonekana kwamba, Man City imekunwa na kiwango cha Grealish na Guardiola anamtaka mchezaji huyo.

Kwa mujibu wa ripoti, nyota wa Barcelona, Messi na mshambuliaji wa Tottenham, Kane wanaonekana hawana uwezekano wa kusajiliwa pale Man City, na Guardiola anamuona Grealish kama ndiye mbadala wao hao.

Ni Kane pekee ndiye mwenye pasi za mwisho nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya England (tisa) msimu huu kuliko Grealish mwenye tano hadi sasa.



# PEPE

## AOMBA RADHI KWA KADI NYEKUNDU

**LONDON, England**

NICOLAS Pepe ameomba radhi baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati Arsenal wakitoka sare ya bila kufungana na Leeds United kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika dakika ya 51 pale kwenye dimba la Elland Road kwa kumbamiza na mpira kichwani, Ezgjan Alioski.

Pepe na Alioski walituma ujumbe wa kutukanwa kwenye mitandao ya kijamii baada ya tukio hilo, ambalo baadaye lililaumiwa na wachezaji wote wa klabu hizo mbili.

Kocha wa 'Washikabunduki' hao, Mikel Arteta, alielezea tukio la winga huyo kwamba "halikubaliki" na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast sasa ameomba radhi kupitia kwenye mtandao wa kijamii kwa kosa lake hilo.

"Jana (juzi) niliiangusha timu yangu na hakuna msamaha kwa tabia yangu," aliandika Pepe kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Kutoka ndani ya moyo wangu napenda kuwaomba radhi mashabiki, wachezaji wenzangu, kocha na watu wote klabuni."

Pepe amekuwa na wakati mgumu msimu huu, kwani mchezo huo dhidi ya Leeds ndio ulikuwa wa pili kwake kuanza kwenye Ligi Kuu ya England.




## MASHABIKI 4,000 KURUHUSIWA KUINGIA VIWANJANI ENGLAND

**LONDON, England**

MAMLAKA ya soka nchini England imepanga kuanza kuwaruhusu mashabiki kuingia viwanjani kuanzia Desemba 2, mwaka huu, katika miji ambayo haipo kwenye athari kubwa ya maambukizi ya virusi vya corona.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Chama cha Soka cha England (FA), kwa kushirikiana na serikali ya Uingereza kimesema kuwa idadi isiyozidi mashabiki 4,000 wataruhusiwa kuingia viwanjani kwenye maeneo yasiyo na kitisho kikubwa cha maambukizi ya corona.

Hadi mashabiki 2,000 wataruhusiwa katika maeneo yatakayoorodheshwa ya Daraja la Pili, lakini hakutakuwa na mashabiki katika maeneo ya Ligi Daraja la Tatu.

Michezo ya ndani inaweza ikabeba mashabiki hadi 1,000 katika madaraja ya kwanza na pili huku uwezo wa mashabiki wa michezo ya ndani na nje ikibaki kuwa asilimia 50.

Hata hivyo, habari njema ni michezo ya ngazi ya chini kabisa, mazoezi ya gym yanaweza kuendelea rasmi ingawa kwa tahadhari kubwa.



## ROONEY SHABIKI WA BARCA, MESSI

**LONDON, Engand**

NYOTA wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney, ameweka wazi kuwa alitaka kujiunga na Klabu ya Barcelona wakati iliporipotiwa kwamba anahitaji kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Msimu wa 2010 wakati akiwa ndani ya Man United, ilielezwa kuwa nyota huyo anahitaji kuondoka ili apate changamoto mpya baada ya kujiunga na timu hiyo msimu wa 2004 akitokea Everton.


Ndani ya Man United aliyodumu hadi msimu wa 2017, alicheza mechi 393 na kufunga mabao 183 na alirejea tena kwenye timu yake ya zamani ya Everton msimu wa 2017-18.

Rooney ameweka wazi kuwa alikuwa anafikiria kucheza ndani ya kikosi cha Barcelona chenye nyota, Lionel Messi.

"Kutoka ndani ya moyo wangu nilikuwa ninapenda kuondoka na kujiunga Barcelona. Nilikuwa shabiki mkubwa wa Barcelona kuliko Real Madrid," alisema Rooney akinukuliwa na Sky Sport.

"Nakumbuka niliwahi kukaa chini nikafikiria kwamba ingekuaje ningecheza timu moja na Messi, Xavi, Iniesta na Busquets, na zama zile Messi hakuwa anacheza kama anavyocheza sasa kama namba 9," alisema.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GRIEZMANN: MESSI ATAKUFA NA MIMI

●●●Nimezungumza naye akatoa kauli hiyo kwa sababu watu wanazungumza vibaya kuwa...

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Antoine Griezmann, amesisitiza mahusiano yake na Lionel Messi ni mazuri, akisema alihisi nyota huyo alikuwa tayari "kufa" kwa ajili yake.

Griezmann amekuwa na wakati mgumu wa kuwa kwenye kiwango chake pale Barcelona tangu alipotua akitokea Atletico Madrid kwa euro milioni 120 mwaka jana.

Mahusiano ya straika huyo na Messi yameibua maswali na Griezmann amebainisha kwamba uamuzi wa kukataa kujiunga na Barca mwaka 2018 ulikuwa ni kwa sababu ya mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

Hata hivyo, Griezmann amesema hana shaka juu ya mahusiano yake na Messi kwa sasa.

"Niliwasili Barcelona baada ya kukataa kuja kabla," alisema akiiambia Movistar.

"Wakati nilipofika kulikuwa na maswali mengi kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, kutoka kwa waandishi wa habari na mashabiki na ndio maana nilipofika niliomba radhi dimbani.

"Kama nilimkosea mtu kwa kile nilichoamua, niliomba radhi uwanjani kwa kuchelewa kutua hapa.

"Nilizungumza na Leo [Messi] wakati nilipokuja na aliniambia ilimuumiza wakati nilipokataa kuja hapa mara ya kwanza, kwa sababu alitamka hadharani na mimi nikasema hapana.

"Na akaniambia atakufa pamoja na mimi kwa sababu watu wanazungumza vibaya na tumeendelea kuwa na mahusiano mazuri tu."

Wakala wa zamani wa Griezmann ambaye ni mjomba wake alibainisha mapema mwezi huu kwamba hana mahusiano mazuri na Messi hasa wakati huu timu ikiwa katika wakati mgumu, nafasi ya 13 kwenye msimamo wa LaLiga.

Lakini Griezmann raia wa Ufaransa amejiweka mbali na kauli ya wakala wake huyo wa zamani.

"Sina mahusiano yoyote na wakala wangu wa zamani tangu siku nilipofunga ndoa. Siku ya harusi yangu nilimualika, lakini hakuja. Ndio maana nikasitisha mahusiano yangu na yeye," alisema.

"Anazungumza vitu ambavyo sijawahi kumwambia, hata baba yangu au dada yangu hawezi kuzungumza na vyombo vya habari bila kuwaambia. Uzuri ni kwamba Leo anajua hilo na anajua namna gani namheshimu na ninavyovutiwa naye."

## KWA UFUPI

### GUARDIOLA AMTAKA GREALISH

PEP Guardiola anataka Manchester City kumsajili Jack Grealish, kwani kiungo huyo wa kati wa Aston Villa na England mwenye umri wa miaka 25 ni kipaumbele chake katika mipango yake ya kuunda kikosi kipya. ***(Independent)***

### HENDERSON HAONDOKI UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza mlinda mlango, Dean Henderson "anataka kusalia Manchester United", licha ya ripoti kuwa mchezaji huyo wa kimataifa mwenye umri wa miaka 23, anataka kuondoka. ***(Mail)***

### LAMPARD AMGANDA GIROUD

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, ambaye anataka kuhamia kwingineko kutafuta fursa ya kuingia kwenye kikosi cha kwanza kabla ya michuano ya euro mwakani, ni "mchezaji muhimu" na amesisitiza anataka abakie Stamford Bridge. ***(Mirror)***

### ISCO YUPO SANA MADRID

REAL Madrid bado haijapokea ofa yoyote kwa ajili ya kiungo wa kati wa Hispania Isco mwenye umri wa miaka 28, ambaye amehusishwa na Manchester City na Arsenal. ***(AS)***

### HAALAND ANAVUTIWA NA EPL

BABA mzazi wa Erling Haaland, Alf-Inge, ambaye ni mchezaji wa zamani wa Nottingham Forest, Leeds na Manchester City, amekubali kwamba nyota huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 20, anavutiwa na Ligi Kuu ya England. ***(Sport 1, via Mirror)***

### MESSI ATABIRIWA MAN CITY

KIUNGO wa zamani wa Manchester City, Trevor Sinclair, anaamini ujio wa nyota wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33 pale Etihad unawezekana baada ya Pep Guardiola kusaini mkataba mpya. ***(Talksport)***

### ERIKSEN AWANIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund iko tayari kuanzisha tena mikakati ya kumsaka kiungo wa kati wa Inter Milan raia wa Denmark, Christian Eriksen, baada ya kuhusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, aliyekuwa Tottenham mapema mwaka huu. ***(Tuttermercatoweb)***

### NUNO AONA MABAO WOLVES

KOCHA wa Wolves, Nuno Espirito Santo ana imani kuwa wataanza kupata mabao na kupunguza shinikizo kwa mchekaji mzuri wa nyavu, mshambuliaji raia wa Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29. ***(Express & Star)***

### QPR KUMUUZA MASTERSON

QPR itamsaka tena beki wa kati na kumuuza mlinzi wa Jamhuri ya Ireland, Conor Masterson mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa Januari. ***(West London Sport)***

### GREALISH KUBURUZWA MAHAKAMANI

NAHODHA wa Aston Villa, Jack Grealish, anakabiliwa na hatari ya kushtakiwa kwa kosa la nne la uendeshaji mbaya wa gari mwaka huu kulikotokea karibu na eneo la kufanya mazoezi la klabu hiyo mwezi uliopita. ***(Birmingham Mail)***

### RYENA AJIFUNGA DORTMUND

KIUNGO wa kimataifa wa Marekani, Giovanni Reyna, mwenye umri wa miaka 18 ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool amesaini mkataba wa muda mrefu na Borussia Dortmund. ***(Team Talk)***

## HABARI MICHEZO

# TFF YAFUNGUKA SAKATA RAIS CAF KUFUNGIWA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Tanzania ikihusishwa na malipo yanayodaiwa kusababisha Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kumfungia kwa kipindi cha miaka mitano Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limetoa onyo kuhusu wote watakaoendelea kusambaza taarifa hizo ilizoeleza kuwa ni za uongo.

Juzi Kamati ya Maadili ya FIFA, ilitangaza kumfungia Ahmad kwa kipindi cha miaka mitano sambamba na faini ya dola za Marekani 220,000 sawa na Sh. milioni 507.9 za Tanzania kutokana na matumizi mabaya ya ofisi pamoja na ufujaji wa fedha, huku Tanzania na Cape Verde zikitajwa kuhusika na mgawo wa fedha kutoka CAF kinyume cha taratibu.

Lakini jana TFF, ilitolea ufafanuzi suala hilo huku ikieleza halitosita kumchukulia hatua za kisheria dhidi ya wote watakaoendelea kusambaza taarifa hizo ilizoeleza kuwa ni za uongo.

Katika taarifa ya TFF, ilianza kwa kueleza: "Ikumbukwe kuwa Mei 2017, Kamati ya Utendaji ya CAF ilipitisha uamuzi kuwa kila mwanachama wake (TFF ikiwamo) kupatiwa mgawo wa dola za Marekani 100,000 ambazo ziligawanywa katika mchanganuo ufuatao;

"Jumla ya dola 80,000 kwa matumizi ya maendeleo ya soka na dola 20,000 kwa Rais wa Shirikisho husika kwa ajili ya kumsaidia katika majukumu yake ya shughuli za mpira wa miguu kutokana na ukweli kuwa hawalipwi mshahara.

"Baada ya mgawo huo wa CAF kuingia kwenye akaunti ya TFF, Rais wa TFF, Wallace Karia, alizielekeza fedha hizo (dola 20,000) zitumike kwa shughuli mbalimbali za shirikisho kutokana na changamoto ya fedha iliyokuwapo. Hakuna fedha ya CAF iliyowahi kuingizwa kwenye akaunti binafsi ya Rais Karia," ilieleza taarifa hiyo ya TFF iliyosainiwa na Ofisa Habari wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo.

Aidha, ilieleza kuwa suala hilo walilitolea ufafanuzi Aprili mwaka huu wakati lilipoibuliwa kwa mara ya kwanza na kwamba wanapenda kusisitiza kuwa fedha tajwa hazikuwahi kulipwa katika akaunti binafsi ya Rais Karia.

"Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Fifa ya kumfungia Rais Ahmad, haikuzungumza chochote kuhusu fedha hizo, dola 20,000 kwenda kwa marais wa wanachama wa CAF. "Hivyo, TFF haitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wote watakaoendelea kusambaza taarifa hizo za uongo," ilieleza.

## MZIGONI LEO...



Kipa wa Azam FC, David Kisu, katika moja ya maandalizi ya Ligi Kuu Bara wakati leo wakiikaribisha Yanga kwenye mechi za ligi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Muuaji Simba aendelea kutakata U/Uhuru

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Ruvu Shooting, Fully Maganga, ameendeleza rekodi yake safi ya kupachika mabao kila akicheza kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, baada ya kufunga tena bao mwishoni mwa wiki, timu yake ikiishindilia Mbeya City mabao 3-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Maganga anayeonekana kuwa na bahati ya kuziona nyavu za Uwanja wa Uhuru, amefunga mabao mara tatu mfululizo, kila timu yake inapocheza dimbani hapo.

Ikumbukwe kuwa Ruvu Shooting kwa sasa inatumia Uwanja wa Uhuru kama wake wa nyumbani, baada ya kufungiwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani. Tangu alipoifunga Simba kwenye uwanja huo, Maganga amekuwa akiendelea kutupia anapocheza dimbani hapo.

"Kikubwa ni mazoezi. Ni mazoezi ninayopewa na kocha wangu Boniface Mkwasa, hasa akinieleza mimi na wenzangu ni jinsi gani ya kucheza kwenye uwanja kama huu wa Uhuru ambao ni wa nyasi bandia," alisema.

Maganga ambaye kwa sasa amefikisha mabao manne kwenye ligi, alianza kufunga bao kwenye Uwanja wa Uhuru Oktoba 26, mwaka huu wakati timu yake ilipoifunga Simba 1-0, Novemba Mosi akifunga tena bao hapo, timu yake ikichakaza Coastal Union mabao 3-1, kabla ya mechi ya mwishoni mwa wiki kuziona tena nyavu uwanjani hapo, Ruvu Shooting ikipata ushindi wa 3-0 dhidi ya Mbeya City.

Maganga ambaye ni nahodha wa Ruvu Shooting, ameiongoza timu hiyo kufikisha pointi 19 zilizoiwezesha kushika nafasi ya nne baada ya kushuka dimbani mechi 11.

# Ngorongoro Heroes hesabu kwa Somalia

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, chini ya miaka 20 'Ngorongoro Heroes', Jamhuri Kihwelo, 'Julio' amesema ana imani na kikosi chake kufanya vizuri katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Julio alisema malengo yao ni kupambana kwenye kila mechi kuhakikisha wanafanya vizuri wakati huu wakielekea kujiandaa kwa mchezo unaofuata dhidi ya Somalia.

Alisema ametumia mechi ya jana kuwasoma wapinzani wao Somalia na kubaini ubora na mapungufu yao kabla ya kukutana nao kwenye mashindano hayo yanayofanyika jijini Arusha.

"Baada ya ushindi mnono dhidi ya Djibout, matokeo hayo hayatufanyi kujiamini zaidi na kutoendelea kujifua kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita," alisema Julio ambaye kikosi chake kiliibuka na ushindi wa mabao 6-1 katika mechi hiyo ya awali.

Ngorongoro Heroes ambayo ipo Kundi A, itashuka tena dimbani kesho kuwavaa Somalia katika michuano hiyo inayoshirikisha nchi tisa.

Nchi zinazoshiriki michuano hiyo ni mwenyeji Tanzania, Kenya, Sudan, Uganda, Sudan Kusini, Somali, Djibouti, Ethiopia na Burundi.

# Lusajo kumbe ni kiboko ya Azam

**Na Saada Akida**

BAO pekee alilofunga wakati KMC FC ikiibuka na ushindi wa 1-0 Jumamosi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, linamfanya Reliants Lusajo kuendelea kuweka rekodi ya kuwa mwiba mkali mbele ya Azam FC kwa kuwafunga misimu miwili mfululizo katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu uliopita Lusajo ambaye alikuwa katika kikosi cha Namungo aliipa ushindi timu hiyo kwa kufunga tena bao pekee wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Azam, kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Katika mechi hiyo alifunga bao hilo dakika ya 60, wakati aliloifungia KMC alilifunga dakika ya 59.

Mshambuliaji huyo ameliambia gazeti hilo kwamba kabla ya mechi kocha wake, Habib Kondo alimpa majukumu ya kuhakikisha anakuwa makini na nafasi anazopata ili kupata pointi muhimu katika mchezo huo dhidi ya Azam.

"Ni kweli nimekuwa na bahati ya kuwafunga Azam, nimetimiza majukumu yangu ya uwanjani, kuhakikisha tunapambana kutafuta pointi muhimu katika kila mechi," alisema Lusajo.

# Michezo

Jumatano Novemba 25, 2020

Nipashe




## TFF YAJITOA SAKATA RAIS CAF KUFUNGIWA

HABARI UK 23

# AZAM, YANGA KUAMUA MBABE WA KILELENI LEO

**Makocha wajigamba kumaliza kasoro mechi zilizopita, kila mmoja akieleza kuwa...**

**Na Saada Akida**

NI ushindi tu ndio utakaoamua mbabe anayestahili kukalia usukani wa Ligi Kuu Bara kwa pointi leo, wakati wababe wanaoshikana shati kileleni kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, Azam FC na Yanga watakaposhuka katika Dimba la Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam kwenye mechi ya raundi ya 12 ya ligi hiyo.

Azam inaongoza ligi hiyo kwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa kutokana kuwa na pointi 25 sawa na Yanga inayoshika nafasi ya pili ikifuatiwa na Simba yenye alama 23, hivyo timu yoyote itakayoibuka na ushindi leo, ndiyo itakayokaa kileleni kwa idadi kubwa ya pointi, lakini sare yoyote ile 'Wanalambalamba' hao wa Bakhressa wataendelea kukaa kileleni kwa tofauti ya mabao.

Ni mechi itakayochezwa saa 1:00 usiku, Azam ikishuka dimbani ikiwa mwenyeji wa pambano hilo, lakini ikiwa na kumbukumbu ya kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya KMC FC katika mchezo uliopigwa Jumamosi iliyopita, wakati Yanga yenyewe itaingia uwanjani, ikiwa haijapata ushindi kwenye mechi tatu mfululizo, baada ya Jumapili iliyopita kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC.

Kocha wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba akizungumzia mchezo huo, amesema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kupambana kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mechi hiyo ili kujiweka katika mazingira ya kubaki kileleni mwa ligi hiyo wanayoongoza kwa tofauti ya mabao.

Alisema alifanyia kazi udhaifu uliojitokeza katika mechi iliyopita ambayo walipoteza, hivyo ana uhakika hayawezi kujirudia tena leo watakapoikaribisha Yanga katika Uwanja wao wa Chamazi.

"Wachezaji wangu wote wapo fiti hakuna majeruhi na tupo tayari kwa mechi yetu hiyo dhidi ya Yanga, utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu wote tunahitaji pointi muhimu, kwetu tunazihitaji sana ili kujiimarisha kubaki kileleni na kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya msimu huu," alisema Cioaba.



Alisema ameimarisha kikosi chake kila idara ikiwamo safu ya ulinzi pamoja na ushambuliaji na wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo ambao utakuwa na ushindani mkubwa kwa timu zote.

Kwa upande wa Kocha wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, alisema amefanyia kazi upungufu uliojitokeza mechi iliyopita, ikiwamo kuwabadilishia mbinu washambuliaji wake ili kuhakikisha wanatumia vema nafasi za hususan ni kwenye umaliziaji.

"Kila mechi ina mpango wake, tulivyocheza dhidi ya Namungo, si tutakavyocheza kesho (leo) dhidi ya Azam, najua itakuwa mechi ngumu, Ligi ya Tanzania ina ushindani mkubwa mechi zote ni tofauti.

"Nimefanyia kazi safu ya ushambuliaji, huku nikiendelea kuwapa majukumu viungo wangu, lakini pia kuwakumbusha mabeki kuwa makini," alisema kocha huyo.

**NIMEREJEA...**



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, akiwa amerejea mazoezini juzi tayari kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta itakayopigwa katika Uwanja wa Anfield leo. Salah alikuwa karantini kutokana na kupata virusi vya corona alipokuwa akiitumikia timu yake ya Taifa ya Misri. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAPEPEA NA MAJEMBE 24

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wamepepea kwa 'mwewe' wa Shirika la Ndege la Ethiopia, wakiwa na kikosi cha wachezaji 24, kuelekea Nigeria tayari kwa mechi yao ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United.

Simba ambayo iliondokea Uwanja wa Ngege wa KIA jana jioni, keshokutwa, Ijumaa itashuka katika Uwanja New Jos uliopo mji wa Jos, Nigeria majira saa nane za huko sawa na saa 10 za Tanzania kwa mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa ngumu kwa kila upande.

**Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, alisema wachezaji alioondoka nao kwa ajili ya mechi ni makipa, Aishi Manula, Ally Salum na Beno Kakolanya, huku mabeki wakiwa ni Shomari Kapombe, Gadiel Michael , Mohammed Hussein 'Tshabalala', Erasto Nyoni, Ibrahim Ame, Joash Onyango, Pascal Wawa na Kennedy Juma.**

Safu ya kiungo walioondoka ni Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Said Ndemla, Rally Bwalya, Hassan Dilunga, Francis Kahata na Clatous Chama, wakati washambuliaji wakiwa ni John Bocco, Meddie Kagere, Miraji Athumani, Bernard Morrison, Luis Miquisson na Ibrahim Ajibu.

Kuhusu mechi hiyo, Sven alisema lengo lake ni kuona wanapata matokeo katika mchezo huo ili kuondoa presha kwenye mechi ya marudiano itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kati ya Desemba 4-6, mwaka huu.

"Wachezaji wangu wote wapo tayari kwa mchezo na kila mmoja anafahamu umuhimu wa kupata matokeo ugenini ili kuondoa presha katika mechi ya marudiano, malengo yetu kwanza ni kufika hatua ya makundi, hivyo tunapaswa kuanza kushinda mechi hii ili kuyafikia," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002